SportPesa
JACKPOT BABA LAO!
TZS. 260,838,830
CHEZA SASA KWA 1000/= TU!
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#



**Basi** lilivyoacha njia na kugonga nyumba, kuua

UKURASA 2



**DIAMOND AKIFA BENDERA JE?**

UKURASA 20


# Nipashe Jumapili

Jumapili Juni 26, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0580988

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


RIPOTI MAALUMU

# Nyuma ya pazia wanandoa kuuana

• **IGP** Sirro, viongozi wa dini, wanasaikolojia wafichua yaliyojificha kwa wapendanao... *Endelea ukurasa 4*



Sheikh wa Mkoa wa Dar es Salaam, Alhad Mussa Salum — IGP Simon Sirro

## YALIYOMO


UKURASA WA 2

**MAVAZI NUSU UTUPU YAWACHEFUA WAZEE**

WAZEE wa Mtaa wa Dome, Kata ya Ndembezi, Manispaa ya Shinyanga wameeleza...

UKURASA WA 8

**IJUE SIRI KUSHAMIRI VITENDO VYA UKATILI**

FAMILIA ni msingi wa maadili mema katika jamii na taifa. Maendeleo...

UKURASA WA 18

**DK. REMMY ALIVYOKIIMBA KIFO KUWAKILISHA MAWAZO YA WENGI**

Remmy amefanya mengi sana, lakini leo nataka kuzungumzia, juu ya yeye kuimba...


## Mbaroni madai ya kufukua kaburi la mwanawe amfufue

UKURASA 2



## Spika atoa maagizo serikalini kikokotoo mafao ya wastaafu

UKURASA 3

**MICHEZO** YANGA SC YAFUNIKA MBEYA UK.24 | **MAONI, KATUNI** UK.6




Katibu Tawala wa Wilaya ya Sengerema, Allan Augustine (kushoto), akipokea msaada wa madawati 190 kutoka kwa Mkurugenzi wa Bodi ya Mgodi wa Sotta (SMCL), Prof. Raphael Chibunda (wa pili kulia), katika kijiji cha Ngoma, mkoani Mwanza, jana. Mgodi pia ulikabidhi lita 200 za Methylated Spirit kwa ajili ya kutoa matibabu katika hospitali za wilaya, vituo vya afya na kliniki. Kulia ni Diwani wa Kata ya Igalula, Raphael Shibiriti. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbaroni tuhuma kutumia wanafunzi kufukua kaburi

**Na Gurian Adolf,**
SUMBAWANGA

JESHI la Polisi mkoani Rukwa linamshikilia Tanga Thadeo (30), mkazi wa Kitongoji cha Kasisiwe, Manispaa ya Sumbawanga, kwa tuhuma za kuwatumia wanafunzi wa Shule ya Msingi Kasisiwe kufukua kaburi la mtoto wake ili amfufue kwa ahadi ya kuwalipa Sh. 10,000.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mjini hapa, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Rukwa, Theopista Mallya, alisema mtuhumiwa huyo aliwataka wanafunzi hao ambao ni wa darasa la nne na sita wafukue kaburi la mtoto wake mwenye umri wa miaka miwili kwa kuwa anaamini alifariki dunia katika mazingira ya kishirikina.

Akisimulia kuhusu tukio hilo lililotokea Juni 21 mwaka huu majira ya mchana, Kamanda Mallya alisema siku ya tukio mtuhumiwa alikwenda katika makaburi ya Kasisiwe kwa lengo la kufukua kaburi la mtoto wake, aliyefariki dunia Juni 16 mwaka huu na kuzikwa siku iliyofuata.

Alisema kuwa baada ya mtuhumiwa kufukua kaburi hilo bila mafanikio kutokana na kuchoka, alikwenda kuwaita wanafunzi wa kiume wa shule hiyo waliokuwa wakicheza mpira karibu na makaburi hayo na kukubaliana nao wafukue kwa ahadi ya Sh. 10,000.

Mmoja wa wanafunzi hao ambaye jina linahifadhiwa, alidai kuwa kabla ya kuanza kufukua, mtuhumiwa aliwataka kwanza wasali na aliongoza sala na baada ya hapo walianza kufukua.

Alisema baada ya kufukua kwa muda mrefu walilifikia jeneza na ndipo mtuhumiwa alipowaambia waache na aliingia kaburini na kulitoa kisha kulifunga mgongoni kwa kutumia shati alilokuwa amevaa na kuwapa fedha waliyokubaliana awali na kuondoka.

Kamanda Mallya alisema baada ya wananchi kugundua kuwapo kwa kaburi lililofukuliwa na mwili kuchukuliwa, walitoa taarifa kwa uongozi wa serikali ya mtaa na kituo cha polisi na kufanikiwa kukamatwa mtuhumiwa huyo.

Alisema baada ya mahojiano mtuhumiwa alikiri kulifukua na kuchukua mwili huo kwa madai kuwa alitaka kumfufua kwa sababu haamini kama kifo chake ni cha kawaida, bali ni cha mazingira ya kishirikina.

Kamanda huyo alisema mtuhumiwa ametenda kosa la jinai kwa sababu kama alitaka kufukua kaburi, alipaswa kuomba kibali cha kufanya hivyo.

# Basi laacha njia, lagonga nyumba, kuua na kujeruhi

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

MTU mmoja amefariki dunia na wengine wawili kujeruhiwa akiwamo mwanafunzi wa shule ya msingi baada ya basi la kampuni ya Geita Express kuacha njia na kugonga nyumba.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Lucas Mwakatundu, alimtaja aliyefariki dunia ni Alon Basili (36), mkazi wa Kijiji cha Mkiwa ambaye mwili wake umehifadhiwa katika Zahanati ya Ikungi.

Alisema ajali hiyo ilitokea juzi saa 2:20 usiku katika Kijiji cha Mkiwa wilayani Ikungi mkoani Singida barabara kuu ya Dodoma-Singida na kulitaja basi hilo ni lenye namba za usajili T 417 CTD aina ya Scania.

Kamanda Mwakatundu aliwataja majeruhi katika ajali hiyo kuwa ni Martha Jeremiah (36), mkazi wa Kijiji cha Mkiwa na Nassoro Abdallah (11), mwanafunzi wa Shule ya Msingi Mkiwa.

Alisema wakati ajali hiyo ikitokea, majeruhi wote walikuwa wamelala ndani ya nyumba hiyo na kwa sasa wanaendelea na matibabu katika Hospitali ya Mtakatifu Gasper iliyoko Itigi Wilaya ya Manyoni.

Alisema uchunguzi wa awali unaonyesha kuwa chanzo cha ajali hiyo ni mwendo kasi na Jeshi la Polisi linamshikilia, Boniphace Machage ambaye ni dereva wa basi hilo kwa uchunguzi zaidi.

# Mavazi nusu utupu yawachefua wazee

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

WAZEE wa Mtaa wa Dome, Kata ya Ndembezi, Manispaa ya Shinyanga wameeleza kuchefuliwa na mavazi ya nusu utupu yanayovaliwa na wasichana huku wakieleza kuwa yamekuwa 'yakiwatega' wanaume na kusababisha kuwafanyia vitendo vya ukatili, ukiwamo ubakaji.

Hayo yalibainishwa na wazee hao juzi katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika Mtaa wa Dome uliokuwa na lengo la kutoa elimu ya kupiga vita biashara na matumizi ya dawa za kulevya, vitendo vya ukatili wa kijinsia na kuimarisha ulinzi na usalama.

Mmoja wa wazee hao, Robert Mwelo, alitaja moja ya sababu ya kuwapo kwa matukio ya ukatili wa kijinsia ni mavazi ya nusu utupu yanayovaliwa na baadhi ya wasichana ambayo huhamasisha wanaume na mwishowe kuwabaka.

"Mavazi ya wasichana wetu ya nusu utupu ndiyo chanzo cha matukio haya ya ukatili. Unajua wanawake ni kama sumaku, wewe unamwona binti kavaa nusu utupu, halafu anatembea huku akitingisha mwili, nikimwona ninaanza kufikiria nimvae nini, maana ananitega. Kwa mavazi haya ya nusu utupu, mtawafunga jela wanaume wengi," alionya.

Mratibu wa Dawati la Jinsia kutoka Jeshi la Polisi Wilaya ya Shinyanga, Brighton Rutajama, alisema jamii inapaswa kuendelea kukemea vitendo vya ukatili wa kijinsia na kutoa taarifa dhidi ya matukio hayo na ushahidi mahakamani ili wahusika wachukuliwe hatua.

Mratibu wa Polisi Jamii Wilaya ya Shinyanga, Osward Nyorobi, aliwataka wazazi mkoani humo kujenga tabia ya kukagua watoto wao kila mara kabla ya kulala ili kuona kama hawajafanyiwa vitendo vya ukatili.

Pia aliwataka wawe makini na wageni wanaokwenda kwenye nyumba zao kwa kuwa matukio mengi ya ukatili wa kijinsia hufanywa na watu wa karibu.

Mwenyekiti wa Mtaa huo wa Dome, Solomoni Najulwa, alisema wameendesha mkutano huo ili kutoa elimu kwa wananchi ili kuacha vitendo vya uhalifu pamoja na ukatili wa kijinsia.

## HABARI KITAIFA




Mkuu wa wilaya ya Mjini, Rashid Simai Msaraka (katikati), akizungumza wakati wa kutangaza azma ya Benki ya NMB kuitunza bustani ya Forodhani na kudhamini mbio za boti Zanzibar kwa kushirikiana na kampuni ya Bima ya Britam, mjini Zanzibar mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Mkuu wa idara ya kadi wa Benki hiyo, Philbert Casmir na Mkuu wa kitengo cha uhifadhi mamlaka ya Mji mkongwe Zanzibar, Mussa Awesu Bakar. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Spika atoa maagizo serikalini kikokotoo mafao ya wastaafu

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, ameitaka serikali kuwaelimisha watumishi wa umma na wananchi kuhusu kikokotoo kwa kuwa baada ya ufafanuzi wa waziri, kumeonekana kuwapo nia njema.

Pia ameitaka serikali kufuata sheria, kanuni na taratibu katika kupunguza mishahara na kushusha vyeo watumishi waliokuwa kwenye nafasi za uteuzi na kuondolewa, ili kusiwe na malalamiko.

Kiongozi huyo wa Bunge aliagiza hayo bungeni jijini hapa juzi baada ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako kutoa ufafanuzi kuhusu kikokotoo kipya cha mafao ya wastaafu kinachopingwa na baadhi ya wadau, wakiwamo wabunge.

Alisema kuwa kikokotoo kipya kinachotarajiwa kuanza Julai Mosi mwaka huu, kimelenga kuweka uwiano na usawa wa mafao baina ya wastaafu, ambapo watumishi wote wa sekta binafsi na umma watalipwa mafao ya mkupuo wa asilimia 33.

"Ninaomba nieleze athari zilizokuwa zinajitokeza kwa kikokototoo cha zamani cha mkupuo wa asilimia 50, mfano halisi ni, kuna mchangiaji katika mfuko ambaye amechangia kwa miezi 467 na michango yake kwa muda wa utumishi wake wote ni Sh. milioni 36.

"Kanuni ya zamani alikuwa analipwa Sh. milioni 129, yaani kachangia Sh. milioni 36 lakini anapata mafao ya mkupuo Sh. milioni 129," alisema.

Prof. Ndalichako alisema wafanyakazi wengine ambao wamechangia Sh. milioni 86 na kufanya kazi kwa miezi 350 kwa kutumia mkupuo wa asilimia 25, wanapata mafao ya mkupuo ya Sh. milioni 54.

"Huyu amechangia Sh. milioni 36 analipwa Sh. milioni 129, huyu amechangia Sh. milioni 86 analipwa Sh. milioni 54," alisema.

Prof. Ndalichako alisema kikokotoo kipya kinaweka wafanyakazi wote wa Tanzania wa sekta ya binafsi na umma, ambao wanasimamiwa na sheria za kazi na ajira zinazofanana kutumia viwango sawa vya ukokotozi wa mafao.

"Kikokotoo kipya kitaondoa utofauti kwa wastaafu ambapo baadhi walikuwa wanalipwa mkupuo wa asilimia 25 wakati wengine walikuwa wanalipwa mkupuo wa asilimia 50, kwa sasa kikokotoo hiki kinasaidia mifuko ya pensheni kuzungumza lugha moja," alisema.

Pia alisema serikali ni sikivu kutokana na malalamiko ya watumishi na wadau kuhusu Kanuni za mwaka 2018 ambapo watumishi wote walikuwa wanalipwa mafao ya mkupuo kwa asilimia 25.

"Serikali ilisitisha kanuni hizo na kuagiza kamati maalum iliyowahusisha wadau wote ambao ni serikali, waajiri na waajiriwa, lengo ilikuwa kuchambua hali ya uhimilivu na uendelevu wa mifuko, makubaliano yaliyofikiwa ndiyo yatakayofanyika kuanzia Julai Mosi, mwaka huu.

Prof. Ndalichako alisema kikokotoo kipya kitawasaidia watumishi kwa kuwa aliyechangia Sh. milioni 86 na mafao yake ya mkupuo yatapanda kuwa Sh. milioni 71 na ataendelea kulipwa pensheni ya kila mwezi ya Sh. 1,840,000 mpaka atakapofariki dunia.

# Balozi Mulamula atumia mkutano wa CHOGM kuitangaza Tanzania

**Na Mwandishi Wetu,** KIGALI

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, ameendelea kutumia majukwaa ya kimataifa kuitangaza nchi na fursa zake kama sehemu ya utekelezaji wa diplomasia ya uchumi.

Katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Madola uliomalizika jana Rwanda ambao ulihudhuriwa takriban na viongozi wa ngazi tofauti wa nchi zote 54 za umoja huo, Tanzania ilitumia fursa hiyo kuhamasisha wawekezaji kuja nchini.

Balozi Mulamula alionekana akifanya mazungumzo rasmi na yasiyo rasmi na mawaziri wenzake wa Mambo ya Nje na hata Mawaziri Wakuu na Marais wa nchini mbalimbali kwa lengo la kuitangaza nchi.

"Rais wetu Samia Suluhu Hassan amefanya mabadiliko makubwa ya kiuchumi na kuboresha mazingira ya biashara, hivyo milango ipo wazi, waambieni wafanyabiashara wenu waje kuwekeza Tanzania kwenye sekta mbalimbali na hasa kilimo ambacho ni moja ya kipaumbele cha serikali," alisema.

Baadhi ya viongozi ambao alifanya nao mazungumzo rasmi ni pamoja na: Waziri wa Mambo ya Nje wa Singapore, Dk. Vivian Balakrishnan; Waziri wa Mambo ya Nje wa India, Subrahmanyam Jaishankar; Waziri wa Mambo ya Nje wa Pakistan, Hina Rabbani Khar; na Mke wa Waziri Mkuu wa zamani wa Uingereza na Mwanzilishi wa Mfuko wa Cherie Blair, Cherie Blair.

Viongozi wakuu aliokutana nao na kuwapa salamu za Rais Samia ni pamoja na: Waziri Mkuu wa Canada, Justin Trudeau; Rais wa Rwanda, Paul Kagame; Rais wa Zambia, Hakainde Hichilema; Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta; na Rais wa Nigeria, Muhammadu Buhari.

Katika mazungumzo hayo pamoja na mambo mengine, Balozi Mulamula alihimiza ushirikiano katika biashara na uwekezaji, mafunzo, usafiri wa anga na utalii. Pia alieleza namna serikali inavyofanya jitihada kuondoa vikwazo vya kibiashara na kuboresha mazingira ya uwekezaji ili kushawishi wawekezaji wengi.

Vilevile, aliziomba Canada, Singapore, India na Pakistan kuleta wawekezaji wengi zaidi Tanzania na hasa katika sekta ya kilimo ambayo ni kipaumbele cha serikali.

Kuhusu utalii, Waziri Mulamula aliziomba nchi hizo kutafsiri filamu ya Tanzania The Royal Tour iliyoongozwa na Rais Samia kwa lugha za nchi zao, ili iwafikie watu wengi zaidi.

Balozi Mulamula alihimiza nchi hizo, hususan India na Singapore kuanzisha safari za moja kwa moja za mashirika yao ya ndege kati ya nchi zao na Tanzania ili kuhamasisha utalii.

Alihimiza ushirikiano na Singapore katika Uchumi wa Buluu kutokana na nchi hiyo kupiga hatua kubwa kwenye eneo hilo, hususan kwenye uendelezaji, usimamizi na uendeshaji wa bandari.

Aligusia pia umuhimu wa kujengeana uwezo hususan katika eneo la rasilimali watu na mafunzo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Wakati wa mazungumzo na Cherie Blair, alieleza utayari wa Mfuko wake wa Cherie Blair Foundation kushirikiana na Tanzania kwenye kuwajengea uwezo wanasheria kuwa na ujuzi wa kutosha wa upatanishi na usuluhishi wa migogoro nje ya mahakama.

Pia alisema mfuko huo upo tayari kuisaidia Tanzania kwa kutoa msaada kwa mawakili katika kesi za kimataifa zinazoikabili Serikali ya Tanzania.

# COSTECH yaipa TALIRI mamilioni

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TUME ya Taifa Sayansi na Teknolojia (COSTECH) imetoa zaidi ya Sh. milioni 400 kwa ajili ya miradi miwili ukiwamo wa uandaaji wa lishe bora ya gharama nafuu kwa unenepeshaji ng'ombe.

Mwingine ni wa ukarabati wa maabara ya utengenezaji na tathmini ya chakula cha ng'ombe katika Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania ( TALIRI), Kanda ya Mashariki Kituo cha Tanga.

Akizindua mradi huo wa uandaaji wa lishe bora juzi, Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Sekta ya Mifugo, Tixon Nzunda, aliipongeza COSTECH kwa ufadhili huo waliotoa kwa taasisi ya TALIRI Tanga.

Nzunda alisema lengo la mradi huo uliofadhiliwa na COSTECH ni kupata lishe sahihi kwa ajili ya kuongeza ubora wa nyama Tanzania pamoja na ukuzaji na uendelezaji kibiashara teknolojia ya lishe ya unenepeshaji ng'ombe na uwezeshaji wa wadau wa tasnia ya nyama.

Meneja Mfuko wa Taifa wa Uendelezaji Sayansi na Teknolojia, Ntufye Mwakigonja, alisema mradi wa maabara umegharimu Sh. milioni 307 na ule wa uandaaji wa lishe bora Sh. milioni 120.

"Fedha hizi zilizotolewa kwa mradi huu wa uandaaji wa lishe bora, zimenunua ng'ombe 30 pamoja na kujenga eneo la majaribio ya ng'ombe wanaonenepeshwa kupitia chakula hicho," alisema.

Mwakigonja alisema kuwa fedha hizo pia zimetumika kulima ekari 12 za mahindi ambayo yametumika kutengenezea lishe.

"COSTECH inaigusa sekta ya mifugo kwa kuzingatia eneo la mapishi kwa sababu mwaka 2020 ilipeleka SUA Sh. milioni 70 kwa ajili ya kubaini matatizo ya malisho ya ng'ombe eneo la Ranchi ya Kongwa Dodoma, baada ya kuvamiwa na gugu," alisema.

Alibianisha kuwa COSTECH pia ilitoa Sh. milioni 400 kwa Kituo cha TALIRI Mpwapwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya maabara.

Mkurugenzi Mkuu wa TALIRI, Prof. Erick Komba, alitaja majukumu ya taasisi hiyo ni kusimamia, kuratibu na kufanya utafiti wa mifugo upande wa Tanzania Bara ikiwamo kubaini, kutathmini na kusambaza teknolojia bora za mifugo.

Alitaja maeneo ambayo TALIRI inafanya utafiti kuwa ni vyakula vya mifugo, malisho, mbari za mifugo, uzalishaji, uzazi, afya ya mifugo, tabia za mifugo na haki za mifugo.

# Nyuma ya pazia wanandoa kuuana

Na Waandishi Wetu

KATIBA ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, mbali na mambo mengine, ina angalizo mahususi kuhusu uhai wa mtu.

Ibara ya 14 ya Katiba hiyo iliyotungiwa Sheria Na. 15 ya Mwaka 1984 (Haki ya Kuishi) inatamka bayana kwamba "Kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata kutoka kwa jamii hifadhi ya maisha yake kwa mujibu wa sheria".

Huku kukiwa na angalizo hilo la kikatiba na kisheria, sasa kunashuhudiwa idadi kubwa ya matukio ya mauaji yanayotokana na wivu wa mapenzi wanandoa na wapendanao wengine wakitoana roho kila kukicha.



Kwa kurejea matukio machache, Mei 28 mwaka huu huko Buswelu mkoani Mwanza, binti wa miaka 28 aliuawa na mumewe kwa kupigwa risasi kwa madai yaleyale ya wivu wa mapenzi. Saa chache baadaye, ikaripotiwa na Jeshi la Polisi kwamba mumewe naye amejiua kwa kujipiga risasi baada ya kutekeleza mauaji dhidi ya mkewe.

Mkoani Shinyanga nako kumeripotiwa tukio la mwanamke kudaiwa kumjeruhi mumewe kwa kumkata sehemu za faragha kwa tuhuma za usaliti.

Huko Tunduru mkoani Ruvuma, mwanamke ameripotiwa na Jeshi la Polisi kufariki dunia na kuacha mtoto wa miezi 11, akidaiwa kuuawa kwa kupigwa risasi kichwani na mchumba wake kutokana na sababu ileile wivu wa mapenzi.

Tukio la mauaji ya aina hiyo pia limetokea wilayani Butiama mkoani Mara, mwanamke mwingine akiripotiwa kumuua mumewe kwa kumchoma kwa kitu chenye ncha kali kwa tuhuma za usaliti.

Hali kadhalika, wilayani Serengeti mkoani Mara ilitolewa taarifa na Jeshi la Polisi ya mume kudaiwa kumjeruhi mkewe kwa kumwingiza panga sehemu za siri, akimtuhumu kuwa na uhusiano na mwanamume mwingine.

Jeshi la Polisi pia limeripoti tukio la mwanamke kumjeruhi mumewe kwa kumkata na wembe sehemu za siri akiwa usingizini na kumsababishia maumivu makali mkoani Ruvuma.

Sasa inaonekana ni matukio endelevu, huku kitendawili kikibaki kuwa 'kuna nini nyuma ya ukatili huu? Pia, kwa nini sasa yanashamiri nchini?

**NYUMA YA PAZIA**

Nipashe Jumapili inatua mezani kwa Zainabu Rashid, mwanasaikolojia kutoka Taasisi ya Ustawi wa Jamii mkoani Dar es Salaam, anayepaza sauti dhidi ya migogoro ya wapendanao isiyotatuliwa.

Zainabu ana ufafanuzi, akitamka: "Sababu inaweza kuwa ni mrundikano wa migogoro. Mtu anapolimbikiza matatizo, yale matatizo ni kama kidonda, kile kidonda usipokitibu kwa wakati kinaendelea kukua na kinapokua, mwisho wa siku kinaweza kukuletea madhara.

"Inapotokea mume amemkosea mke wake au mke amemkosea mume wake kwa muda mrefu na amekaa bila kusuluhisha jambo hilo, inatengeneza kama kidonda kinakua.

"Kitakapolipuka, akili ya binadamu ina namna fulani ya kufanya kazi kulingana na vile ulivyotunza taarifa. Hivyo, mtu anaweza kufanya jambo bila kujua, lakini ni matokeo ya uzoefu alioupata baada ya kufanya jambo fulani.

"Kuna kitu kinaitwa haiba, mwingine anaweza kusamehe, mwingine ni rahisi kusahau, mwingine anatunza. Mwisho wa siku anakuja kufanya tukio kubwa kwa sababu ametunza matukio mbalimbali.

"Kitu kingine ni malezi, hasa ya kihisia. Familia nyingi hazilei watoto katika ukuaji wa kihisia katika kuhimili hisia zao, kwa sababu siyo kila haki yake atapewa. Kwa hiyo, wanandoa au wapenzi wanaingia kwenye mauaji kwa sababu wameshindwa kuhimili hisia zao za hasira au wivu."

Shekhe wa Mkoa wa Dar es Salaam, Alhad Mussa Salum, hayuko mbali katika kukimulika kilicho nyuma ya pazia kuhusu mauaji miongoni mwa wapendanao.

Kiongozi huyo wa kiroho anasema: "Ni wimbi tu la shetani linapita, kwa sababu mambo kama haya huwa yanatokea kwa kipindi fulani kisha yanapotea. Lakini kama ni elimu, viongozi tunatoa juu ya uharamu wa kujiua na kuua mtu mwingine."

Akiwa mkoani Iringa juzi, Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Simon Sirro, alilaani vitendo vya mauaji vinavyofanywa na baadhi ya watu kwenye jamii, yakiwamo yanayohusisha wapendanao.

Alisema jeshi hilo litaendelea kuwachukulia hatua za kisheria watu watakaobainika ikiwamo kuwafikisha mahakamani, akisisitiza kuwa kumekuwa na matukio ya mauaji aliyoyaita ya ovyo ambayo yanasababishwa na ukosefu wa maadili na hata imani za kishirikina.

"Tufike mahali tuseme basi, tujue kuwa Mungu yupo na kwamba kuna siku tutakwenda kuwajibika," IGP Sirro alionya.

**NINI KIFANYIKE?**

Ili kukabiliana na tatizo hilo, Mwanasaikolojia Zainabu ana angalizo kwa wazazi na walezi kuwa chimbuko la mauaji haya miongoni mwa wapendanao ni makosa yaliyochagizwa na wazazi na walezi kutowajibika katika malezi ya watoto wao.

"Wazazi wazingatie malezi ya ukuaji wa watoto kihisia, watoto wanakua na hisia tangu wanapozaliwa. Kwa hiyo, mpaka wanapokuwa watu wazima, watakuwa wanajua namna ya kuhimili hisia zao," anasisitiza.

Mwanasaikolojia huyo pia ana rai yake kwa jamii, akiitaka kuchukua hatua inapoona mtoto anakwenda kinyume cha maadili mema yaliyowekwa kwenye jamii anayoishi.

Nipashe Jumapili inaporejea kwa Shekhe wa Mkoa wa Dar es Salaam, Alhad Salum, kupata mustakabali wa tatizo la mauaji yanayotikisa ya wapendanao nchini, anashauri:

"Inawezekana hata mawaidha yanayotokana na viongozi wa dini siyo watu wote yanawafikia huko maeneo waliko. Kwa hiyo, inatakiwa kuongeza vyombo vya mawasiliano katika vijiji, kwenye miji mbalimbali na watu wawe wanafuatilia vyombo hivi ambavyo vitawaelimisha kwa namna moja au nyingine.

"Pia watu wafuate misingi yao ya dini na miongozo yao ya kiimani ili kujiepusha na majaribu ya shetani."

Ni muhimu wanandoa wawe wepesi kujifunza, kujikosoa, kujisahihisha na kuombana msamaha pale mtu anapohisi kumkosea mwenzake. Ni vema ifahamike kuwa, hakuna ndoa yenye afya njema bila zoezi la msamaha. Msamaha ni dawa ya furaha ya familia. Msamaha ni muhimu kwa afya yetu ya kihisia na kuendelea kuishi kwa heri. Asiyeomba msamaha na asiyesamehe hana amani katika nafsi yake na hawezi kuwa na ushirika na Mungu. Pia, mtu wa aina hiyo hawezi kuwa na uhusiano mwema na binadamu mwenzake.

Watu wasioomba msamaha na wasiosamehe ni wagonjwa wa kimwili, kihisia na kiroho. Siku zote huteseka na kuishi kwa vinyongo na roho ya visasi na maangamizi. Bila msamaha, familia inakuwa uwanja wa migogoro, ngome ya uovu na maafa.

Mchungaji wa Kanisa la Kilutheri la Kiinjili Tanzania (KKKT), Dk. Mlyuka, anasema migogoro ya ndoa ni adui wa maendeleo kwa kuwa maendeleo na ustawi wa familia na Taifa unategemea ndoa imara.

Dk, Mlyuka ambaye pia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Tanzania Marriage and Child Care (TaMCare) inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi, anasema ni muhimu kila mwanandoa ajiheshimu, atambue nafasi, wajibu na mipaka yake katika ndoa ili kuifanya ndoa kuwa baraka.

Vilevile, IGP Sirro katika kusaka mwarobaini wa mauaji miongoni mwa wanandoa na wapendanao, hayuko nyuma kuishauri jamii, akitamka: "Kama unaona mwanamke amekuzingua, unaachana naye. Pia, kama mwanamume amekuzingua, unaachana naye, maisha yanaendelea kama kawaida.

"Na pia kinadada muangalie ni mwanaume gani unaolewa naye, siyo kila mwanamume ni mwanamume bora, kuna wanaume wengine ni mizigo na kuna wanawake wengine ni mizigo pia."

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kilirekodi matukio ya mauaji ya kikatili 20, yakiwamo ya wapendanao, kwa mwezi Januari mwaka huu.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa kituo hicho, Anna Henga, matukio hayo yaliripotiwa katika mikoa ya Mtwara, Rukwa, Njombe, Katavi, Mwanza, Dodoma, Ruvuma, Dar es Salaam na Mara.

**■Imeandaliwa na Joyce Ammi, Lydia Sylivester na Wilbgeorge Bahati (SJMC).**



## Matairi yasiyojazwa upepo yapunguza ajali barabarani

**Na Moshi Lusonzo**

AJALI za barabarani zinazosababishwa na uimara hafifu wa magurudumu kwa mabasi na malori ya kusafirisha bidhaa zimepungua baada ya asilimia 98 ya vyombo hivyo kutumia matairi yasiyojazwa upepo.

Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Exaud Kigahe, aliyasema hayo juzi wakati wa maadhimisho ya miaka 30 ya ushirikiano kati ya kampuni mbili za Superdol na Michelin jijini Dar es Salaam.

Kigahe alisema uwekezaji katika matairi hayo ya kisasa umeboresha sekta ya usafirishaji kutokana na wanaotumia vyombo hivyo kuwa na uhakika wa usalama wa maisha na mali zao wawapo barabarani.

Alisema serikali inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, imeweka kipaumbele cha maendeleo ya watu na ukuaji wa uchumi, hivyo uawekezaji wa ndani na nje unaofanywa katika kuboresha sekta ya uchukuzi lazima ulindwe kwa nguvu zote.

"Kutokana na uwekezaji wa matairi haya yasiyotumia upepo katika magari ya abiria na mizigo, matukio ya ajali yamepungua na kwa sasa watu wanauhakika wa kusafiri salama na kusafirisha bidhaa zao kwa wakati," alisema.

Kigahe alisema kupitia ushirikiano wa kampuni ya Superdol ya nchini na hiyo ya Michelin kutoka Ufaransa, mafunzo ya kujenga uelewa wa matumizi salama ya barabara kwa madereva yametolewa kwa wamiliki wa magari na maofisa wa polisi wa usalama barabarani. Mwenyekiti wa Superdol, Seif Ally Seif, aliipongeza serikali kwa kuwaunga mkono katika lengo lao la kuhakikisha sekta ya usafirishaji inakuwa ya kisasa na kuachana na matumizi ya vifaa vya bei rahisi ambavyo vingi husababisha madhara kwa jamii kutokana na kutokuwa imara.

"Katika miaka 30, kama washirika tuliamua kuhamasisha na kutoa mafunzo kuhusu matumizi ya matairi salama ambayo yanaepusha madhara. Ninaishukuru serikali kwa kuunga mkono jambo hili kiasi ambacho asilimia kubwa ya vyombo vya usafirishaji, vinatumia matairi yasiyo na upepo," alisema.

Seif alisema kampuni hizo mbili zitaendelea kutoa huduma kwa kiwango bora na kutimiza wajibu wao wa kuelimisha umma kuhusu matumizi ya barabara.




Mkuu wa Gereza la Segerea, SSP Hamis Lissu (wa pili kulia), akiangalia msaada wa katoni za taulo za kike, Televisheni, sabuni na maziwa ya Lactogen, baada ya kukabidhiwa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya kuleta tumaini kwa wafungwa Tanzania (TPHF), Mchungaji Lucas Mwimo (wa tatu kulia), kwa ajili ya mahabusu na wafungwa wanawake na watoto wao, gerezani hapo, Segerea, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Katibu wa TPHF, Mohamed Majengo. **PICHA: JOHN BADI**

# Tanzania yamwagiwa sifa kasi mapambano tabianchi

**Na Romana Mallya**

BALOZI wa Uingereza wa Masuala ya Mabadiliko ya Tabianchi kwa Afrika na COP26 wa Kanda ya Mashariki ya Kati na Afrika, Janet Rogan, ameipongeza Tanzania kwa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa kufanyia kazi baadhi ya maazimio ikiwamo matumizi ya nishati mbadala na uvunaji wa hewa ukaa.

Akizungumza juzi jijini Dar es Salaam baada ya kumaliza ziara yake ya siku nne, Rogan alisema amefurahi kuitembelea Tanzania kwa mara ya kwanza na ameridhishwa na hatua mbalimbali ambazo nchi inazichukua katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Alisema akiwa Tanzania, amepata fursa ya kutembelea miradi mbalimbali ya uhifadhi mazingira na kufanya mazungumzo na serikali, taasisi za nishati na mazingira na kuona namna jamii inavyofikiwa na fursa zitokanazo na miradi hiyo. "Serikali na wadau wengine wanafanya kazi kwa bidii katika ahadi na maazimio ya COP26 Glasgow. Usalama wa chakula na maji, kilimo na nishati mbadala zitakuwa mada kuu katika COP27 Misri, hivyo Uingereza na Tanzania tuendelee kushirikiana pamoja," alisema.

Balozi wa Uingereza nchini Tanzania, David Concar, alisema nchi yake itaendelea kushawishi kampuni na taasisi kupunguza matumizi ya hewa ukaa kwa kutafuta soko lake.

Kwa mujibu wa taarifa ya ubalozi huo, ziara ya Rogan imezingatia maazimio ya Tanzania baada ya mkutano wa 26 wa mabadiliko ya tabianchi uliofanyika Uingereza mwaka jana (COP26) na uwezekano wa upanuzi wa biashara ya kaboni.

Pia imezingatia urejeshaji wa misitu, ushiriki wa sekta binafsi katika kukabiliana na mabadilio ya tabianchi na kupata Fedha za Kimataifa za Hali ya Tabianchi (GCF), mchakato wa kitaasisi wa Tanzania kuhusu hatua za mazingira na namna Uingereza inavyoweza kuwa sehemu ya utekelezaji huo.

Ziara hiyo pia imebeba uimarishaji wa uwekezaji na ushirikiano wa Uingereza na Tanzania kwa hatua za utekelezaji wa lengo la 13 la Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG13) kufikia COP26 na mikakati ya COP27 utakaofanyika Misri mwezi Novemba mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa ya ubalozi huo, Janet wakati wa ziara yake, amekutana na Waziri wa Nishati, Januari Makamba, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, na Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Abdallah Mtawi.

Ilisema wamekutana kwa lengo la kuimarisha uhusiano wa nchi hiyo na Tanzania katika kufikia 'net zero' (sifuri) ifikapo mwaka 2050 na umuhimu wa ushiriki wa Tanzania katika COP27.

Balozi huyo pia alipata fursa ya kuzungumza na kampuni na taasisi za nishati na mazingira katika kuelewa nafasi ya uwekezaji wa Uingereza katika sekta hiyo, matatizo na mabadiliko ya biashara katika muktadha wa kufikia malengo ya maendeleo.

# SUMAJKT kuzindua kitabu cha miaka 41

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMAJKT) linaadhimisha miaka 41 tangu kuanzishwa kwake mwaka 1981 sambamba na kuzindua kitabu maalum kinachoeleza mafanikio na mipango yake ya baadaye.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mkoani Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa SUMAJKT, Kanali Petro Ngata, alisema maadhimisho hayo yanatarajia kufanyika kwa siku tatu kuanzia Jumatano ya wiki ijayo (Juni 29) mkoani humo.

Alisema yatafanyika sambamba na maonyesho ya 46 ya biashara ya kimataifa katika viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere, maarufu Sabasaba, na mgeni rasmi anatarajiwa kuwa ni Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Stergomena Tax.

"Kimsingi SUMAJKT linajivunia kusherehekea miaka 41 tangu kuanzishwa kwake kwani limefanikiwa kutimiza malengo ya kuanzishwa shughuli za JKT na kusaidia katika kujenga uchumi wa nchi.

"Katika kilele cha maadhimisho, shirika litazindua kitabu cha maadhimisho ya miaka 41, ambapo historia, miradi ya shirika, mafanikio, matatizo, na mipango ya baadaye imeelezwa humo, hii ni katika kuweka kumbukumbu vizuri kwa ajili ya vizazi vijavyo." alisema.

Mkurugenzi huyo alisema shirika limefanikiwa kuchangia Pato la Taifa kwa kutoa gawio serikalini na kodi stahiki kupitia kampuni zake tanzu.

Pia alisema limefanikiwa kutekeleza miradi mbalimbali ya kibiashara na ile ya huduma yenye maslahi ya taifa, ikiwamo ujenzi wa ukuta wa kuzunguka mgodi wa madini wa tanzanite, Mirerani mkoani Manyara, kujenga mji wa kiserikali jijini Dodoma.

Alisema SUMAJKT imeshiriki ujenzi wa Ofisi za Rais Ikulu Chamwino, Dodoma pamoja na uzio wake wenye urefu wa kilomita 27 mwaka 2021 na mradi wa nyumba 41 katika Ikulu mwaka 2020, majengo sita ya wizara na jengo la Tume ya Uchaguzi Tanzania (NEC), Makao Makuu.

Kanali Ngata alisema shirika hilo limefanikiwa kutoa ajira kwa vijana wa KItanzania kupitia kampuni na miradi yake ikiwamo Kampuni ya Ulinzi SUMAJKT Guard hadi sasa imetoa ajira kwa vijana zaidi ya 16,000.

"Shirika limekuwa likisaidia vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa, kujifunza stadi za kazi kupitia shughuli zake mbalimbali za uzalishaji mali ikiwamo kilimo, ufugaji, ujenzi, utengenezaji wa samani na bidhaa za ngozi.

Alisema shirika limeona huu ni wakati sahihi wa kufanya maadhimisho hayo kwa mara ya kwanza, ikiwa ni kutambua hatua kubwa iliyopigwa katika maendeleo yao.

Kanali Ngata alisema mara ya mwisho shirika lilipata ruzuku kutoka serikalini mwaka 1988, hivyo kama watendaji wa SUMAJKT hawana budi kujivunia hatua iliyofikiwa sasa.

Alisema shirika lilitumia fedha zake lenyewe na kupata mafanikio katika sekta ya kilimo, viwanda na ujenzi hadi hapo shughuli za JKT ziliposimamishwa mwaka 1994.

"Hali hii iliathiri kiwango cha uzalishaji mali kwani nguvu kazi ya vijana ilipungua na kupelekea shirika kutegemea nguvu kazi ya maofisa na askari katika kuendesha miradi hususani ile ya kilimo, iliyohitaji vijana.

"Mwaka 2001 serikali iliporejesha tena shughuli za kuchukua vijana wa kujitolea shughuli za SUMAJKT pia zilianza kukua," alifafanua.

Pia alisema mafanikio inayojivunia ni pamoja na kutoa ajira kwa vijana zaidi 14,000 ambao wanafanya kazi za ulinzi kupitia kampuni ya ulinzi ya SUMAJKT.

"Katika kuunga mkono juhudi za serikali za kufikia uchumi wa kati wa viwanda mwaka 2025, SUMAJKT imeboresha viwanda vilivyopo na kuanzisha vipya na sasa inamiliki viwanda vitano ambavyo ni SUMAJKT Garments, SUMAJKT Chang'ombe Furniture, SUMAJKT Leather Products, SUMAJKT Bottling na SUMAJKT Mlale Mills," alivitaja.

Pia alisema wamefanikiwa kuanzisha miradi tisa ya huduma na biashara katika kipindi cha miaka 41 pamoja na kununua vitendea kazi kupitia faida wanazopata.

Kiongozi huyo alitumia nafasi hiyo kuwakumbusha Watanzania kushiriki mchakato wa sensa ya watu na makazi iliyopangwa kufanyika Agosti 23 mwaka huu.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uendeshaji wa masoko ya chakula nchini umulikwe

**MASOKO** ya chakula yana mchango mkubwa katika kuimarisha afya na kusaidia upatikanaji wa mahitaji ya chakula.

Vilevile, masoko hayo ni sehemu ya biashara ambayo huwapatia wafanyabiashara kipato cha kukidhi maisha yao ya kila siku.

Kwa kutambua hilo, ni wazi kwamba suala la usafi wa masoko ya chakula ni muhimu kwa afya za wafanyabiashara na watumiaji wa vyakula vinavyouzwa katika masoko hayo.

Mwongozo wa Shirika la Afya Duniani unaolenga kuchochea usimamizi bora wa chakula unaonyesha kuwa katika kila watu 10, mmoja huugua magonjwa yanayosababishwa na kula chakula kisicho salama kila mwaka.

Pia, watoto milioni 1.8 walio chini ya umri wa miaka mitano huumwa kipindupindu, huku asilimia 70 ya ugonjwa huo husababishwa na kula chakula chenye vijidudu vinavyotokana na uchafu.

Wakati kukiwa na tahadhari hiyo kiafya, hali ya masoko ya chakula nchini bado si ya kuridhisha, baadhi yakiwa katika hali ya uchakavu na uchafu.

Kinyume cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) ya mwaka 1982 inayozipa Mamlaka za Serikali za Mitaa jukumu la kusimamia na kuboresha afya ya jamii, imeripotiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwamba mamlaka hizo zimeshindwa kusimamia ipasavyo usafi katika masoko.

Halmashauri zimeshindwa kutenga kiasi cha fedha kinachokusanywa kutoka katika masoko kama mapato ili kugharamia usafi wa masoko ya chakula.

Kulingana na agizo la Ofisi ya Rais - TAMISEMI, kila halmashauri inatakiwa kutenga asilimia 15 ya mapato yanayopatikana kutoka katika masoko ili kutekeleza shughuli za maendeleo, marekebisho na usafi katika masoko husika.

Kwa kipindi cha miaka minne (2016/17-2019/20), halmashauri (10) zimefichuliwa na CAG zilikusanya jumla ya Sh. bilioni 23.48 kutoka katika masoko ya chakula, lakini zilirudisha Sh. milioni 697, sawa na asilimia tatu tu ya makusanyo yaliyotoka katika masoko, ili kutekeleza shughuli za usafi katika masoko hayo.

Uchunguzi wa CAG pia umebaini kuwapo na idadi kubwa ya wafanyabiashara katika masoko zaidi ya uwezo wa masoko hayo, hivyo kusababisha uzalishaji mkubwa wa taka na uchakavu wa miundombinu.

Nipashe, tukiwa wadau wa usalama wa afya na mazingira, tunazikumbusha mamlaka husika kurekebisha dosari tajwa ili wananchi wasiendelee kununua vyakula katika masoko ambayo si salama kiafya. Masoko hayo yanaweza kusababisha milipuko ya magonjwa yanayotokana na uchafu kama vile kipindupindu.

Nipashe pia tunazishauri mamlaka husika kuchukua hatua stahiki dhidi ya uchakavu wa miundombinu unaoathiri zaidi wafanyabiashara wa jinsi ya kike ambao ndiyo watumiaji wakubwa wa masoko ya chakula kwa kukosa maeneo bora ya kujisitiri na kufanya biashara.

Vilevile, Nipashe tunaishauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuhimiza halmashauri zote nchini kuhakikisha zinafuata agizo linalozitaka kutenga asilimia 15 ya mapato yanayopatikana katika masoko, ili kutekeleza shughuli za maendeleo, marekebisho na usafi katika masoko yao.


Ili kuwe na ufanisi katika hilo, tunafikiri kuna haja ofisi hiyo iwachukulie hatua za kinidhamu watendaji wote wa halmashauri ambao hawatatenga asilimia 15 ya mapato yanayopatikana katika masoko ili kutekeleza shughuli za maendeleo, marekebisho na usafi katika masoko hayo.

Pia, Halmashauri zitakiwe kusimamia kikamilifu uanzishwaji wa kamati za usimamizi wa masoko, utungaji wa sheria ndogo za usimamizi wa usafi wa masoko na uimarishaji, ufuatiliaji wa uendeshaji wa masoko.

Hii iende sambamba na kuwapa wananchi taarifa ya mapato na matumizi yatokanayo na makusanyo ya masoko, ili wawe wanahoji pale inapobidi na kupatiwa majibu sahihi juu ya usimamizi wa rasilimali hizo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Tuanze sasa kutoa 4,000/- kwa walimu

Na Sabato Kasika

**WALIMU** ni miongoni mwa watumishi wa umma ambao wanapitia shida nyingi ambazo huenda wakati mwingine zinasababisha kupunguza ufanisi wao kazini.

Kazi ya ualimu mara kadhaa imekuwa ikielezwa kuwa ni wito, lakini ni vyema wakaandaliwa mazingira yatakayowawezesha kutekeleza wito wao bila manung'uniko.

Ili kuondoa malalamiko, si vibaya wakawezeshwa kimafunzo, ukuzaji wa taaluma, kuboreshewa mazingira ya kazi ambayo yatasaidia kufanya kazi kwa uwezo wote na wanafunzi wanaowafundisha wanufaike na ujuzi wanaopewa madarasani.

Lakini, pia suala la uboreshaji wa maslahi ni mojawapo ya mambo ya msingi ambayo yamekuwa ni kilio chao cha muda mrefu.

Ninaamini kwamba, hatua hiyo na nyingine nyingi, zinaweza kusaidia ufufuaji wa elimu ikiwa zitatekelezwa kikamilifu, huku wakishirikishwa kwa kila hatua inayohusu maslahi yao.

Kwenye jambo hili, wapo wadau mbalimbali wa elimu ambao wamekuwa wakitamani kuona walimu wanaboreshewa mishahara, marupurupu na motisha kazini.

Profesa Kitila Mkumbo ni miongoni mwao na anashauri njia inayoweza kusaidia kuwa ni pamoja na kuwajali walimu.

Akichangia hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu ya mwaka 2022/23 bungeni hivi karibuni, alishauri serikali kurudisha utaratibu wa kuwaongezea motisha.

Katika ufafanuzi wake, anasema walimu wanatakiwa kupewa posho ya Sh. 4,000 kwa siku na kwamba kwa mwezi mmoja anapaswa kulipwa Sh. 100,000 kiasi ambacho anabainisha kuwa serikali inakimudu.

Msomi huyo pia anagusia suala la kufuta kada ya maofisa elimu kata ili kuziba pengo la uhaba wa walimu katika shule mbalimbali nchini, kwamba ni muhimu kupunguza utawala katika elimu ili kuimarisha menejimenti ya shule.

Profesa Mkumbo anatamani kuona maofisa elimu kata hao wakienda darasani kufundisha, huku serikali ikiajiri walimu 20, 000 hadi 30,000 kwa mwaka ili kuziba pengo la uhaba wa walimu.

Katika ushauri wake huo, anaeleza kuwa muda wa mafunzo ya ualimu uongezwe kutoka miaka mitatu hadi minne ili wanapohitimu, wawe wameiva kikamilifu na wafundishwe kwa vitendo.

Ushauri huo ungefaa kupewa uzito unaotakiwa, hasa kwa kuzingatia kwamba walimu ni wahusika wakuu wa juhudi za kufufua na kufikia elimubora iliyo jumuishi na yenye usawa kwa kila mwanafunzi, katika kila hali.

Wao ndiyo wanaofundisha viongozi wa leo na baadaye, madaktari na wataalam wa kila fani hivyo ni suala la kuwawezesha kwa kila hali ili wafanye kazi kwa moyo mkunjifu na kwa ufanisi.

Lakini pia walimu pia wamekuwa kiini cha elimu, kuanzia kutumia teknolojia kwa ubunifu hadi kutoa msaada wa kijamii na kihisia kwa wanafunzi wao ili wafikie malengo waliojiwekea kwenye elimu.

Hivyo, kama itakuwa vigumu kuwawezesha kwa kila kitu, lakini suala la motisha ya Sh. 4,000 kwa siku lianze ili lisaidie angalau kuwafanya waendelee kuwa na moyo wa kujituma hata kwenye mazingira magumu.

Ikumbukwe kuwa zipo baadhi ya shule zina walimu wachache, huku idadi ya wanafunzi ikiwa kubwa, ninaamini kwamba katika mazingira hayo, utendaji kazi wao hauwezi kuwa na ufanisi.

Hivyo, jambo la muhimu ambalo lingesaidia kuwafanya wakabiliane na mazingira hayo wakati serikali ikiendelea kuajiri wengine, ni kuwapa motisha ya Sh. 4,000 kama anavyoshauri Prof. Mkumbo.

Kuwapo kwa posho hiyo kunaweza kusaidia kumaliza msuguano kati ya wazazi na walimu ambao wamekuwa wakituhumu baadhi ya walimu kuwa wanalazimisha wanafunzi kufanya 'twisheni' ili wapate fedha.

Pamoja na hayo, hatua iliyochukuliwa na serikali ya kuondoa ada kidato cha tano na sita, ni nzuri, lakini hatua zaidi zingeelekezwa kuboresha maslahi ya walimu ili wafanye kazi yao bila manung'uniko.

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# Tusiruhusu jambo hili liendelee



Na Pascal Mayalla

**Kutamka wazi kuwa kila Mtanzania ana haki ya kugombea nafasi yoyote ya uongozi kwa mujibu wa ibara ya 21 ya Katiba, bila kulazimishwa kudhaminiwa na chama cha siasa, hivyo mtu anaweza kugombea kama mgombea binafsi.**

LEO ninaendelea na ile mada ya kuhusu Haki za Kikatiba, zilizotolewa na Ibara moja ya Katiba, halafu zikaja kuporwa kwa kuchomekewa vifungu vinavyopora haki hiyo na ibara nyingine

Haki ninayoizungumza hapa ni haki ya kuchaguliwa iliyotolewa na Ibara 21 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, jinsi ilivyokuja kuporwa na sharti la mgombea uongozi wa umma, kudhaminiwa na chama cha siasa, hivyo kuipora kabisa ile haki iliyotolewa na Ibara ya 21.

Mchungaji Mtikila (Mungu amweke mahala pema peponi), mwaka 1993, alifungua kesi Na. 5 ya 1993, alifanya kusudi kubwa kukipinga kifungu hiki na Mahakama Kuu kupitia kwa Jaji Lugakingira (Mungu amweke mahala pema peponi), ikatamka wazi na bayana kipengele hicho ni batili na kinakiuka Katiba ya JMT ya mwaka 1977, hivyo kifutwe na kutoa haki kwa kila Mtanzania ana haki ya kushiriki kugombea uongozi

Baada tu ya Mtikila kushinda kesi, serikali ikafanya mambo mawili makubwa. Kwanza, ilikata rufani kuipinga hukumu ya Jaji Lugakingira! Pili, ilipeleka bungeni kwa hati ya dharura, Sheria Na. 34 ya mwaka 1994 kufanya marekebisho ya Katiba ya JMT na kukichomeka kipengele hicho ndani ya katiba, hivyo kuibatilisha ile hukumu ya Jaji Lugakingira.

Mchungaji Mtikila licha ya kuwa ni mwanasiasa, Mwenyekiti wa chama cha siasa cha DP (Democratic Party), alikuwa ni mtu wa Mungu kiukweli kabisa, kwa sababu hakukubali katiba yetu ichezewe, hivyo akafungua kesi nyingine Na. 10 ya mwaka 2009 kupinga marekebisho hayo ya 8 katiba na kuyaita ubatili.

Katika kesi hiyo, Mchungaji Mtikila aliomba mambo mawili makuu: (a) Mahakama itamke Ibara 39 na 67 za katiba zilizorekebishwa na marekebisho ya 8 kwa sheria Na. 34 ya mwaka 1994, ni batili na kinyume cha katiba.

(b) Kutamka wazi kuwa kila Mtanzania ana haki ya kugombea nafasi yoyote ya uongozi kwa mujibu wa ibara ya 21 ya Katiba, bila kulazimishwa kudhaminiwa na chama cha siasa, hivyo mtu anaweza kugombea kama mgombea binafsi.

Mahakama Kuu chini ya majaji watatu (majaji watatu kisheria inaitwa Half Bench); Manento, Masati na Mihayo, wakayakubali mambo yote ya Mchungaji Mtikila na kumpa ushindi tena kwa kutamka marekebisho hayo ya katiba ni batili!

Lakini serikali yetu ya wakati huo, ikakata tena rufani na safari hii Mahakama Kuu ikakaa 'Full Bench' chini ya majaji saba, wakiongozwa na Jaji Mkuu mwenyewe, Agustino Ramadhani, akisaidiwa na Jaji Munuo, Jaji Msoffe, Jaji Kimaro, Jaji Mbarouk, Jaji Luanda na Jaji Mjasir, ambapo tarehe 17 mwezi Juni 2010, ikatoa hukumu.

Tena Mahakama haikuwa peke yake, bali iliwaita mabingwa wabobezi watatu wa sheria na katiba kuisaidia, hawa wanaitwa marafiki wa mahakama, kwa Kiingereza ni 'friends of the Court, kisheria wanaitwa Amicus Curiae, hivyo ma- Amicus Curiae hawa, Othman Masoud (baadaye akawa Mwanasheria Mkuu Zanzibar, sasa ni Makamu wa kwanza wa Rais Zanzibar), Prof. Palamagamba Kabudi na Prof. Jwan Mwaikusa.

Uamuzi wa Mahakama Kuu ya Rufani uliamua ifuatavyo, hapa ninaomba ninanukuu: "So as to let the will of the people prevail as to whether or not such [independent] candidates are suitable. We are definite that the Courts are not the custodians of the will of the people. That is the property of elected Members of Parliament".

Hapa Mahakama ya Rufani Tanzania ilijivua jukumu la kuilinda katiba.

Kitendo cha Mahakama kujivua jukumu la kuwa 'the custodian of the will of the people' Hakuna 'will of the people' kubwa kuliko katiba! Kama katiba imetoa haki fulani, halafu Bunge likatunga sheria kuifuta haki hiyo, ilitegemewa mahakama kutumia mamlaka yake ya "checks and balance".

Nia ya Bunge haliwezi kutunga sheria inayokwenda kinyume cha katiba! Mahakama ikatamka haiwezi kuliingilia Bunge! Mahakama ya Rufani ikaamua kuwa Mahakama haina mamlaka ya kuliingilia Bunge, katika vipengele vya katiba, kumaanisha kwa vile marekebisho hayo ya 8 yamefanywa na Bunge, hivyo ni Bunge ndilo lirekebishe kipengele hicho!

Yaani Bunge litunge sheria batili inayokwenda kinyume cha katiba, kisha kipengele cha sheria hiyo batili kikachomekewa ndani ya katiba kwa mabadiliko ya katiba kwa hati ya dharura!. Mahakama Kuu inasema huu ni ubatili, Mahakama ya Rufani inasema "hatuwezi kuliingilia Bunge!

Katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015, baadhi ya majaji wakaonyesha wazi ni makada wa vyama vya siasa! Jaji Mkuu mstaafu aliyeongoza jopo hilo, alichukua fomu kutaka kugombea urais!

Baadhi ya wale ma 'amicus curiae', naamini tunawajua na tunawaona na ukada wao! Unategemea nini kama wakuu wa mhimili wa mahakama mara tu baada ya kustaafu wanageuka makada!

**Wasalaam**
**0754 270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Watanzania hebu sasa tumrudie Nyerere kwa hili



Na Joseph Kulangwa

HISTORIA ya nchi hii haidanganyi aslani. Ukiambiwa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, alipigania uhuru wa nchi hii, hata akavuka mipaka akaingia nchi zingine hususan za Afrika kusaidia kupatikana uhuru, amini.

Inatwambia kuwa Mwalimu alikuwa tayari kuchelewesha uhuru wa Tanganyika mpaka nchi zingine ikiwamo Kenya, zipate uhuru wao. Alikuwa si tu mzalendo kwa nchi yake, bali pia kwa nchi zingine.

Hakuishia hapo, bali alitaka pia Afrika iwe huru na ikiwezekana iungane iwe nchi moja kama ilivyo Marekani na kuwa na nchi iitwayo Afrika. Yote hayo yalitokana na kutambua kuwa bila umoja Afrika haitafika kokote.

Hata tulipopata uhuru wa Tanganyika mwaka 1961, hakulala, akahamia kusini mwa Afrika, kutafuta uhuru wa mataifa hayo, si Angola, si Msumbiji mpaka Afrika Kusini kwenyewe, Namibia na kwinginekо huko na mpaka uhuru ukapatikana.

Sina uhakika kama Nyerere katika jitihada zake hizo alikuwa akijinufaisha binafsi, lakini sitakubali mtu akinishawishi kuamini hivyo, kwa sababu sioni ni nini alichokuwa akikitafuta zaidi ya haki na utu wa binadamu.

Alifanikiwa kwa kiasi kikubwa, alikuwa na mchango katika kuanzishwa Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU) mwaka 1963, lakini pia akachangia kuzaliwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) mwaka 1967 na hatimaye Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) mwaka 1980 na kurekebishwa mwaka 1992.

Kote huko Nyerere akishirikiana na wenzake, viongozi wa mataifa ambayo baadaye yalikuja kupata uhuru, akapambana na kuona Afrika ikienda pamoja sambamba na Jumuiya zilizokuwa zimeundwa kikanda.

Nyerere hakusita kwenda nchi ya Kiafrika alikosikia kuna migogoro, akienda kupatanisha kama si kusuluhisha. Ndiyo sababu akakubali kupokea wakimbizi na kuwahifadhi mpaka hapo mataifa yaliyokuwa katika mapigano yalipotulia.

Mataifa mengi duniani yalitushangaa Watanzania, kwa kupokea maelfu ya wakimbizi na kuwahifadhi kwenye kambi maalum Kigoma, Tabora na hata Rukwa, wengi wakitoka Kongo, Rwanda na Burundi.

Tanzania tukajenga jina kubwa duniani, kwamba tulikuwa tukipigania haki za wanyonge, tukipinga utawala wa kiimla. Kumbukeni tulivyomfurusha Nduli Dyamini (Iddi Amin Dadah) wa Uganda na majeshi yake.

Mnakumbuka jinsi tulivyopeleka majeshi yetu Anjouan na kuwafurusha waasi waliokuwa wanakikalia kisiwa kile na kuwanyamazisha moja kwa moja? Kumbukeni vizuri tu tuliyoyafanya kwa waasi wa Kongo-M23.

Tukaendelea na juhudi hizo za kupigania haki, kwa kupeleka majeshi ya kulinda amani katika mataifa mbalimbali duniani na kufanya kazi iliyotukuka, bila kusikia hata siku moja majeshi hayo yamefanya uonevu au uporaji.

Nia njema ya uongozi wa Tanzania, moyo wa upendo miongoni mwao na dhamira ya kweli ya kuhakikisha haki inatendeka ni vitu vilivyotufanya kupata mafanikio katika mambo yote hayo, kupambana na maadui wa ndani na nje kwa mafanikio makubwa.

Mwalimu Nyerere alifariki dunia akiwa anapatanisha Burundi ambako kulikuwa na mgogoro, akisafiri hapa na pale huku akiugulia, lakini akitaka dhamira yake ikamilike na Afrika iwe Bara la amani kama alivyokusudia yeye.

Mmeshasahau kuwa Mwalimu alikuwa Mwenyekiti wa Tume ya Nchi za Kusini mwa Afrika-South South Commission? Bila shaka mnakumbuka, na ndiyo sababu hata makao makuu ya ukombozi wa Afrika yakawa Dar es Salaam. Mnamkumbuka Hashim Mbita? Shauri yenu kama mmemsahau.

Leo mimi ninaona kama Tanzania tumeanza kupoteza hatamu za kupambania amani Afrika. Ninajiuliza kulikoni, mbona yale yaliyokuwa yakifanywa na Mwalimu Nyerere kwa mataifa rafiki na ndugu kama Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) ni kama yamekosa mrithi?

Zamani tukisikia M-23 wamevamia Goma, Mashariki mwa DRC haraka tumelaani na kushiriki vikao vyote vya kupanga mikakati ya kukabikiana na uasi huo na mara moja kupanda ndege na kila kitu chetu kwenda kupambana nao.

Ndiyo tunaonekana kuguswa, lakini si kwa uzito uule. Ni kwa nini? Mbona tunataka kuacha kumuenzi Baba wa Taifa, ambaye inaonekana sasa kumuenzi kiaina ifikapo Oktoba 14 tu ya kila mwaka na kusahau kuwa ametuachia alama ya watu wenye upendo na mshikamano kwa binadamu wengine.

Kwamba ni sisi tuliokuwa tayari kuahirisha uhuru wetu ili jirani apate wa kwake kwanza, ili tukae meza moja tuungane na kuwa kitu kimoja? Inakuwaje sasa, tunajivuta sasa? Hebu tumrudie Nyerere jamani. Alamsiki!

# Ijue siri kushamiri vitendo vya ukatili



FAMILIA ni msingi wa maadili mema katika jamii na taifa. Maendeleo yanahitaji watu waadilifu. Uadilifu huo unajengwa kuanzia ngazi ya familia.

Tunaishi katika jamii ambayo kuna migogoro na kuvunjika kwa ndoa nyingi. Hali kadhalika, ombwe la malezi ya watoto ni kubwa katika jamii yetu ya leo, kwani wazazi wengi hawana muda na watoto wao.

Hali hii inaathiri sana makuzi ya watoto na kuchangia ongezeko la vitendo vya ukatili dhidi ya watoto. Ukatili ni tatizo la kimaadili, hivyo, vitendo vya ukatili wa kijinsia vinapoongezeka katika jamii ni kiashiria cha mmomonyoko mkubwa wa maadili.

Tabia na mienendo yetu inajengwa katika familia. Wanasaikolojia wanasema, zaidi ya asilimia 6 ya wewe na mimi tulivyo leo ni matokeo ya makuzi wakati wa utoto. Hivyo, watu wakatili wametengenezwa katika familia. Ni vema ieleweke wazi kuwa, jukumu la kujenga jamii na taifa letu ama kulibomoa, tunalo sisi wazazi, walezi na wanajamii.

Wakati umefika sasa jitihada za kupinga vitendo vya ukatili dhidi ya watoto zisiwe za kutoa matamko, kutengeneza mabango, fulana au vipeperushi tu na kutafuta umaarufu, bali jitihada hizi lazima ziende sambamba na dhana nzima ya malezi katika ngazi ya familia. Ustawi wa taifa unaanzia nyumbani kwa kuwa uhai wa taifa unategemea uhai wa familia.

**Malezi ya mtoto**

Mtoto ni malezi. Kauli mbiu ya Siku ya Mtoto wa Afrika mwaka huu wa 2022 inasema, "Tuimarishe ulinzi wa mtoto; tokomeza ukatili dhidi yake". Mlinzi namba moja wa mtoto ni mzazi. Ni wajibu wa baba na mama kuwapa watoto malezi bora. Malezi bora ni ulinzi, ufunguo na urithi wa maisha kwa mtoto.

Taasisi, jamii na taifa bora la kesho linategemea malezi bora yanayotolewa na taifa bora la leo. Malezi bora huanzia katika ngazi ya familia.

Malezi bora ndiyo mwelekeo sahihi wa maisha ya mtoto, kwani kesho bora ya mtoto inajengwa na leo bora ya wazazi bora.

Familia ni msingi na kitengo kinachomtengeneza mtoto kiroho, kimwili na kitabia (attitudes). Vitengo vingine kama taasisi za dini au shule husaidia tu na kuendeleza msingi uliojengwa na wazazi.

Kwa hiyo, kazi ya vitengo vingine inaweza kuwa nyepesi au ngumu kutegemea na jinsi kitengo cha msingi yaani familia kilivyotunza wajibu wake wa malezi. Wazazi wanapaswa kuwa mfano bora wa matendo, kauli na mienendo yao. Watoto wa leo ni raia na viongozi wa kesho; ndiyo watakaokuwa sifa au aibu kwa wazazi wao, kwa familia yao, kwa jamaa na taifa lao.

Waswahili wanasema, "mtoto umlevyo ndivyo akuavyo". Ni wajibu wa wazazi kuwapa watoto wao malezi yatakayowaandaa kuishi maisha ya kumpendeza Mungu na binadamu wengine. Wazazi msikwepe wajibu wa kukemea pale inapobidi. Watoto wote wasioadibishwa na wenye tabia mbaya ni udhia, mzigo, karaha, na fedheha kwa wazazi na jamii. Ukimdekeza mwanao iko siku atakuaibisha na kukusababishia maumivu usiyoyatarajia.

Mtoto mwenye malezi mabaya atakuwa na maisha magumu hapo mbeleni. Watu wasiowajibika, magaidi, wakatili, wanyanyasaji, vibaka, walevi, kundi la watoto linalojiita, "Watoto wa Ibilisi" na "Panya Road" kama ilivyoripotiwa na vyombo vya habari siku za hivi karibuni, wahuni wa kila aina tulionao leo ni matunda ya malezi mabaya.

Migogoro ya ndoa huchangia katika kutengeneza kizazi cha watu wakatili. Migogoro ya ndoa huwakosesha watoto haki ya kufurahia maisha na kuwafurahia wazazi wao.

Akili (brain) ya watoto inavurugwa kwa sababu ya kubebeshwa maumivu na matendo mabaya ya wazazi wao.

Wazazi wengine wamekuwa na tabia mbaya ya kuwashirikisha watoto tofauti zao au matatizo yao, wakisahau kwamba kwa kufanya hivyo ni sawa na kuwalisha watoto sumu inayowaua kimakuzi pole pole. Kukosekana kwa utu na vitendo vya ukatili ni matokeo ya tabia ambazo huzalishwa na ndoa zenye migogoro.

**Wazazi wawe na muda na watoto**

Wazazi msiridhike tu na kule kuwapatia watoto wenu mambo ya ulimwengu huu. Watoto wenu wanahitaji uwepo wenu wakionja hisia, mapigo ya mioyo yenu, hali ya kujali na kuthamini maendeleo ya kiroho, kimwili, kiimani, kisaikolojia na kadhalika.

Upendo na muda unaopatikana kwa ajili ya watoto wenu ni zawadi kubwa isiyoweza kuthaminishwa na chochote. Mtoto hahitaji tu baba au mama bali anahitaji baba au mama anayejali na anayepatikana nyumbani. Baba na mama wasiwe kiwanda cha kuzalisha watoto na kuwatelekeza pasipo kuwajibika katika malezi.

Kuwa baba au mama ni jukumu kubwa. Kwa hiyo, ni muhimu sana wazazi wafahamu majukumu waliyonayo kwa watoto wao ili kujenga familia na jamii bora. Maadili mema ni uhai kwa familia, jamii na taifa.

Hatuwezi kuendelea kiroho, kimwili, kiuchumi, kisiasa na kijamii pasipokuwa na maadili yanayompendeza Mungu na binadamu wenzetu.

Hivyo, ili tuwe na taifa imara la watu waadilifu na wasio wakatili, lazima mkazo uwekwe katika malezi ngazi ya familia. Baba na mama waishi katika upendo na kuonyesha tabia ya kila mtu kumjali mwenzake ili kutokupandikiza roho ya ukatili kwa watoto wao.

**Elimu dunia na elimu ya kiroho**

Watoto waliozaliwa kama raia wa dunia hii wanapaswa kutambua kuwa uraia wao halisi uko mbinguni. Hivyo, lazima watoto waandaliwe kwa ajili ya hatima hiyo pia. Jitihada za kuwapatia watoto wetu elimu dunia ni muhimu sana ziende sambamba na kuwapatia elimu ya kiroho (kuhusu Mungu) ili watoto hawa wawe baraka sasa na hapo baadaye. Malezi bora ni uwekezaji na urithi muhimu katika maisha ya mtoto.

Tutengeneze kizazi chenye kumpenda Mungu na binadamu mwingine. Vinginevyo tutakuwa na watu ambao ni mzigo usiobebeka kwa familia yenyewe, jamii na taifa kwa ujumla. Waswahili wanasema, "mkunje samaki angali mbichi".

Ukiwa mzazi au mlezi unaalikwa uwashirikishe watoto imani yako kuhusu Mungu, upendo wako kwa jirani na tumaini la maisha mema ya baadaye.

**Uhuru wa kuamua**

Tuwape watoto wetu uhuru wa kuamua, kuchagua, kutoa mawazo kuhusu maisha yao, lakini watoto wapewe uhuru wenye mipaka. Uhuru usio na mipaka matokeo yake ni vurugu, fujo na uharibifu. Tuwasaidie watoto na vijana wetu wasiendekeze tama, starehe na anasa, kiu ya mali na utajiri pasipo uwajibikaji wa kutosha. Tuwasaidie kufahamu kuwa maisha mazuri yanatengenezwa kwa kuwa na nidhamu binafsi ya maisha, juhudi, subira na uvumilivu, na kumtanguliza Mungu katika kila jambo.

**Familia ni shule**

Familia ni kitovu cha malezi, shule ya Neno la Mungu, sala na kitalu cha maadili mema. Wazazi tunapaswa kuwa mfano mwema kwa watoto wetu, kwani watoto hujifunza zaidi kwa kuona na kusikia.

Ikumbukwe kwamba, siku zote matunda mema hutoka katika mti bora. Watoto wenye malezi bora; walioelimishwa kumcha Mungu watakuwa na utii, upendo, na msaada mkubwa kwa wazazi wao katika umaskini na uzee wao na kufanyika baraka kwa watu wengine pia. Suala la malezi katika ngazi ya familia ni ajenda muhimu katika jitihada za kupinga vitendo vya ukatili dhidi ya watoto.

**■Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066].**

# MAISHA

JUNI 26, 2022
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili




Ukurasa 13

**Nguo za Kigiriki zinazoendelea kutamba**



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Hii ndiyo nyumba imara



Ukurasa 12

**HARUSI**




# Miguu kupasuka tatizo linalotibika kirahisi

Ukurasa 14

# WATOTO

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA








| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | K | A | N | D | A |
| ■ | I | ■ | ■ | U | ■ |
| T | M | K | ■ | N | ■ |
| ■ | B | ■ | I | G | A |
| ■ | I | ■ | ■ | U | ■ |
| N | A | N | G | A | ■ |

## AMSHA AKILI


TUMIA RANGI YA NJANO NA KIJANI TU



## TOA TOFAUTI 5




## PAKA RANGI



@MSAMBA

## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
IMO, ALA, KINDA, PWANI, NYUMBA, POLISI

## CHEKA



Alichokifanya daktari

MTOTO John alikuwa akizungumza na mama yake mara baada ya kumaliza kupitia masomo yake ya shule.

Wakiwa katika mazungumzo, John alimwambia mama yake jinsi anavyotakiwa kuwa msanii mkubwa wa uimbaji wa muziki. Alisema ndoto yake hiyo haitatimia kama hatakuwa na sauti nzuri kama za wanamuziki wakubwa.

**John:** Mama nataka kuwa kama Diamond, Ali Kiba au Marioo ambao wana sauti nzuri.

**Mama:** Sawa mwanangu weka bidii katika uimbaji na pia uwe na sauti nzuri.

**John:** Lakini mama mwalimu wetu alinitisha sana eti ukiwa na sauti nzuri inaweza kumtoa nyoka pangoni

**Mama:** Hapana hakuwa na maana hiyo kama unavyoamini, yeye alimaanisha kwamba uwe na sauti nzuri ambayo inaweza kumfanya kila mtu kukusikiliza na kuipenda.

**SWALI**
Samaki Pweza ana idadi ya mikia mingapi?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Tahadhari kwa nini fedha haitaki kuhodhiwa

***KARIBU tena msomaji wangu tumalizie sehemu ya mwisho ya mada yetu kuhusu siri ya fedha katika maisha yetu ya kila siku. Nilieleza mambo mengi ikiwa ni pamoja na ukweli kwamba fedha siyo kwa ajili ya matumizi bali kwa ajili ya kuwekeza.***

Kwa kadri unavyopunguza matumizi na kuongeza uwekezaji, ndivyo utakavyoongeza fedha zako. Leo tuangalie, katika mazingira hayo, jambo gani lifanyike?

Nirudie tena kusema kuwa kila mtu Mungu amempa kipawa kitakachomwezesha kufanikiwa katika maisha. Hivyo, kijue kipawa chako na kukitumia.

Tambua kuwa fedha ina tabia ya kuingia na kutoka. Hii ni siri ya tano unayopaswa kuielewa na kuzingatia, baada ya siri nne nilizoeleza awali, ili kujipatia mafanikio.

Mpenzi msomaji, hebu jaribu kukumbuka fedha zote zilizopitia mikononi mwako hadi leo zimekwenda wapi na zimekupa faida gani. Hautafanikiwa kujiongezea kipato kama una roho ya kuhodhi fedha, zikiingia hautaki zitoke.

Kwa sababu fedha zina tabia ya kuingia na kutoka, hautaweza kuzizuia na zitatoka wala hautajua zimekwenda wapi! Ili kuondokana na changamoto hii ya kushindwa kuzuia fedha zisitoke, zitengenezee njia sahihi ya kutoka ambayo itakutengenezea kipato.

Hata hivyo, unatakiwa kuwa na zaidi ya bajeti. Kwa sababu fedha ina tabia ya kutaka kuongezeka, na wakati huo huo ina tabia ya kuzunguka na siyo kukaa mahali pamoja, tayarisha miradi makini hata kama huna mtaji.

Utaratibu huu utakusaidia sana kwani fedha itakapokujia na wakati wa kutoka utakapofika, itakwenda kwenye miradi uliyotayarisha. Maana yake ni kwamba, tayarisha uwekezaji kabla ya kupata fedha.

Usingoje upate fedha kwanza ndipo utayarishe uwekezaji kwa sababu fedha zina tabia ya kuingia na kutoka. Siku zote jipange ili fedha zinapotaka kutoka ziingie kule unakotaka kuzielekeza.

Kumbuka, roho ya kuhodhi fedha ni roho ya uchoyo, yaani unyimivu. Mwenye kuhodhi fedha huishi maisha duni ingawa ana fedha nyingi alizozificha mahali.

Hadi sasa nimeeleza jinsi ya kuongeza kipato chako kwa kutumia fedha kwa njia sahihi. Ili kuendelea kuzitumia fedha kwa faida ni muhimu pia nikupe tahadhari kuhusu kujipatia fedha kwa njia za mkato.

Tahadhari ya kwanza, epuka kupenda fedha. Kupenda fedha kumefananishwa na shina linalobeba kila aina ya uovu! Kupenda fedha (philarguria- kwa Kiyunani) ni zaidi ya kuhitaji fedha.

Kupenda fedha ni kuabudu fedha, kuipa kipaumbele katika maisha yako zaidi ya Mungu! Agizo la Mungu la nani wa kumpenda, "Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote, na kwa akili zako zote; na jirani yako kama nafsi yako".

Unapopenda fedha, upendo wako kwa Mungu unapungua, wakati wewe kujua. Unapojikuta katika hali ya kufanya uamuzi ndipo utakapojua ni nani unayempenda zaidi, fedha au Mungu.

Tahadhari ya pili, afya ni bora kuliko fedha. Baadhi ya watu katika harakati ya za kutafuta fedha wamepuuza umuhimu wa kutunza afya zao. Kumbuka fedha inaweza kukupatia matibabu lakini siyo uponyaji.

Mwenye hekima mmoja toka huko Asia ya Mashariki, alishangazwa na tabia ya watu kutafuta fedha kwa bidii pasipo kuzingatia afya zao na kuishia kutumia fedha hizo kujitibu!

Tengeneza utaratibu wa kuboresha afya yako. Mungu anataka tuwe na afya njema ndio sababu ameweka kinga mbalimbali ndani ya miili yetu.

Maradhi yamekuwa ni shida kubwa kwenye familia nyingi, hasa kutokana na gharama kubwa za matibabu. Panga ratiba ya mazoezi, pata bima ya afya, tenga fungu la matibabu.

Fedha kwa sababu ni ubunifu wa mwanadamu na siyo kitu kilichoumbwa na Mungu, haitaki kutawaliwa au kuhodhiwa. Mtu yeyote mwenye fedha nyingi ni rahisi kuvamiwa na roho ya kuhodhi ili azitumie kutawala wasio nazo.

Na kwa sababu fedha haitaki kuhodhiwa, hutafuta njia ya kuondoka na hii huchangia matajiri wengi kufilisika pasipo kujua sababu. Ukiwa na hekima ya kuwekeza kwa watu na siyo kuwadharau, kuna wakati utakuja kuvuna ulichopanda!

***Tuishie hapa. Naamini umejifunza kitu kuhusu siri ya fedha. Je, una maoni? Tuma ujumbe 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Manispaa, TRA wachukue hatua kudhibiti hoteli hizi

UNAPOSAFIRI kwa basi kwenda mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, Kanda ya Kati na Kanda ya Ziwa, lazima utapita mkoani Morogoro na kwa wanaotumia magari ya alfajiri kwenda Songea, Njombe, Mbeya na Ruvuma lazima wanasimama kupata kifungua kinywa kwenye 'Mji Kasoro Bahari'.

Kwa wanaokwenda Mwanza, Musoma, Shinyanga, Bukoba, Kahama na kwingine kwa mwelekeo huo wanapotoka Dar es Salaam, kituo cha kwanza kwa ajili ya huduma za kijamii ni mjini Morogoro.

Kama hilo haitoshi, wanaokwenda mikoa ya jirani kama Dodoma hasa kwa magari yasiyo ya alfajiri, wanasimama kupata chakula cha mchana au cha jioni kwenye moja ya hoteli za mkoa huo kutegemeana na makubaliano baina ya dereva na wamiliki wa hoteli.

Kwa ujumla, unaposafiri kwenda mikoa mingine husuan ya Kanda ya Kaskazini na Kusini huduma za vyakula ni za kuridhisha sana kuanzia usafi wa eneo husika na vyakula, lakini siyo kwa njia ya Morogoro.

Hoteli zote ambazo mabasi yanasimama ili abiria 'wachimbe dawa', wapate huduma ya chakula na mapumziko kwa ujumla siyo za kuridhisha kabisa, hali inayozua maswali mengi kwa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kwamba huwa haioni hayo yote?

Kuanzia huduma ya vyoo ni kuchafu na vibovu kiasi cha kuziweka hatarini afya za wasafiri kwa kuwa hakuna anayefuatilia, mwenye biashara huamua anavyotaka kwa kuwa hakuna ukaguzi.

Vyakula vinauzwa bei ya juu, vinywaji vinauzwa mara mbili hadi tatu ya bei na wakati mwingine abiria ananunua kwa kuwa anahitaji na ndilo eneo pekee alilofikishwa na dereva wa basi husika.

Ninatambua kwenye kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuna Ofisa Afya ambaye moja ya majukumu yake ni kufuatilia usafi wa maeneo yote ya biashara, hasa hoteli na migahawa inayotumiwa na watu wengi, kisha kuchukua hatua, ikiwamo kufunga biashara husika kwa anayebainika kutokidhi vigezo.

Migahawa na hoteli ninayoizungumzia mjini Morogoro iko kilomita chache kutoka iliko Manispaa ya Morogoro. Swali ninalojiuliza wanafanya ukaguzi hadi kwenye vyoo, wanaona vingine havina milango na ni chakavu kupita kiasi au wanaacha bora liende na kukusanya kodi pekee?

Ni muhimu sana Manispaa ya Morogoro ikajali afya za wananchi, kama ambavyo maeneo hayo yanawaingizia fedha kama chanzo cha mapato, wanao wajibu wa msingi kufuatilia huduma zinazotolewa humo kama zinaridhisha.

Ni lazima hatua zichukuliwe ili mazingira ya hoteli na migahawa iboreshwe au kujengwa upya. Kama mtu anataka kuwekeza kwenye huduma hizo, afanye uwekezaji wa kuridhisha na kukidhi vigezo vyote vya afya kuliko wananchi kuingizwa kwenye matatizo.

Kama maeneo haya wanatoza fedha zaidi ya bei halisi ya bidhaa husika, kwanini wanashindwa kuboresha maeneo yakawa mazuri na ya kuridhisha kuanzia huduma za vyoo, chakula na vinywaji?

Maana yake ni kwamba hakuna ufuatiliaji wa serikali, ndiyo maana kimebaki kuwa chanzo cha mapato pekee pasi na ufuatiliaji wa kama huduma zinazotolewa zinakidhi matakwa ya kiafya kwa mujibu wa sheria.

Wasafiri ni watoto, vijana, umri wa kati na wazee ambao ni mchanganyiko wa wanaume na wanawake, wote wanatumia vyoo visivyoridhisha na ambao wako hatarini zaidi kupata maradhi ya njia ya haja ndogo ni wanawake na watoto.

> **"Kama maeneo haya wanatoza fedha zaidi ya bei halisi ya bidhaa husika, kwanini wanashindwa kuboresha maeneo yakawa mazuri na ya kuridhisha kuanzia huduma za vyoo, chakula na vinywaji?**

Lazima hatua zichukuliwe tuone mabadiliko kuliko hali kuachwa ilivyo, serikali isiishie kukusanya mapato pekee, bali kujiridhisha na kusimamia usafi wa maeneo husika. Kama inashindikana wachukue hatua kwa mujibu wa sheria.

Hoteli nyingi za Kanda ya Kaskazini mteja anaponunua chochote anapewa stakabadhi ya EFD, lakini kwa hizi za Manispaa ya Morogoro, kwa uzoefu wangu wa kusafiri njia hiyo sijawahi kupewa stakabidhi, maana yake hata Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapoteza mamilioni ya shilingi ambayo yangeingia kwenye kapu la Taifa na kutekeleza miradi ya maendeleo.

Kama hoteli za Kamda ya Kaskazini imewezekana kuweka mashine za EFD, basi hata Morogoro na mikoa mingine ambayo mamia ya wasafiri hutumia huduma, kuwe stakabadhi hizo muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu.

***Mungu ibariki Tanzania***

# HARUSI





Ilikuwa vifijo na nderemo walipofunga ndoa Salum Baline Mawona na Fatma Mohamed Sharifu iliyofanyika Jijini Mwanza tarehe 10/6/2022 na kufuatiwa na sherehe iliyofanyika katika ukumbi wa Dunken Jijini Dar





# MITINDO






# Nguo za Kigiriki zinazoendelea kutamba

UNAWEZA kusema kwamba dunia ya mitindo ya mavazi kwa wanawake ilianzia nchini Ugiriki. Hii inatokana na ukweli kwamba aina ya magauni yote yenye umaarufu chanzo chake kinatoka nchi hiyo.

Unapowaona wanawake waking'ara kutokana na magauni yao marefu, yenye mitindo ya kushangaza, usifikiri yametoka hewani tu, bali ni matokeo ya watu wa nchi hiyo ambao walitaka kuona wanawake wakiwa na mwonekano wa kipekee.

Zipo nguo ambazo zina shingo za V, au sehemu kubwa ya maeneo ya mabegani yapo wazi, basi hiyo ni mitindo ya Kigiriki ambayo inazidi kupendwa kila kukicha duniani kote.

Jamii ya Kigiriki ya kale ilitaka kuwaona wanawake wana asili ya urembo, ndio maana hata nguo zao zilishonwa katika ustadi mkubwa ambao unaweza kueleza vyema kuanzia tumboni, shingoni hadi kichwani.

Mitindo mingi ya magauni yanayovaliwa katika sherehe mbalimbali yamebuniwa katika mfumo wa Kigiriki yanayoelezea zaidi urembo na kung'ara.

Hata aina ya viatu vinavyovaliwa sasa ni matokeo ya wabunifu wa kale ambao kila wakati walitaka kuona mwanamke yupo sawa na Malaika kutokana na mvuto wake.



UREMBO

# Miguu kupasuka tatizo linalotibika kirahisi

KUWA na miguu au visigino vilivyopasuka maarufu kama gaga ni moja ya sababu inayoonyesha katika mwili kuna upungufu wa virutubisho.

Japo wengi wetu tumekuwa na mitazamo kwamba, visigino kupasuka ni ishara ya mtu kutojali usafi, lakini ukweli ni tatizo la kiafya linaloendelea ndani ya mwili.

**Sababu za kupasuka gaga**

Miongoni mwa sababu zinazoweza kumfanya mtu apasuke visigino ni pamoja na, ngozi kuwa kavu sana na kuifanya ishindwe kustahimili kutanuka na kusinyaa.

Pia upungufu wa virutubisho mwilini, mfano madini ya Zinc, Vitamini E pamoja na mafuta ya omega 3 husababisha ngozi kupoteza uimara wake na kuifanya ipasuke kirahisi.

Baadhi ya magonjwa kama vile matatizo ya kisukari, homoni na umri mkubwa huchangia utendaji kazi wa mifumo mbalimbali katika mwili wake kupungua kiufanisi.

**Njia za kutibu**

Chukua mchanganyiko wa maji ya uvuguvugu na chumvi, unapoanza kusafisha unyayo weka miguu katika maji ya moto kiasi, kwa muda wa dakika tano kisha anza kusafisha kwa kusugua hakikisha mabaki ya ngozi laini katika miguu yako.

Weka miguu katika mchanganyiko wa maji pamoja na asali, ambayo husaidia kulainisha ngozi ya unyayo wako pamoja na kuondoa michubuko iliyopo katika unyayo.

Futa miguu yako kwa kitambaa safi kuanzia katika vidole vyako. Usipokausha vyema hupelekea kupata fangasi na kufanya miguu kunuka unapokuwa umevaa viatu vya kudumbukiza.

Watu walio chanika miguu wanashauriwa kutumia viatu vya wazi kwa muda mrefu huku ukizingatia taratibu za usafishaji wa nyayo.



MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Furahia mbuzi choma

WATU wengi wamezoea kula nyama ya mbuzi kwenye baa na maeneo mengine kwa sababu hawajui namna ya kuchoma na kuwa laini kama vile zinakuwa za kwenye baa.

Katika safu hii wiki hii tunaelezana njia rahisi za kuchoma nyama ya mbuzi laini na utafurahia nyuma hii.

**Mahitaji**

Unahitaji uwe na vitu vifuatavyo ili kuweza kukamilisha kuchoma mbuzi wako.

Miongoni mwa vitu hivyo ni vitunguu swaumu vilivyosagwa, tangawizi iliyosagwa, mafuta kiasi cha nusu Lita, beef masala, Celery isage pamoja na swaumu.

Mahitaji mengine ni chumvi kiasi kidogo maana nayo ikizidi sio nzuri, stopiliwili ya kuchoma mbuzi, mkaa na mbuzi ambae tayari ameshachomwa na kutolewa uchafu wa tumboni.

**Namna ya kuandaa**

Jinsi ya kutengeneza marination yako kwa ajili ya kuchoma mbuzi wako.



Chukua celery, unachanganya swaumu, mafuta, tangawizi, chumvi na beef masala na ziache kwa muda nyama ilainike.

Baada ya hapo unatengeneza sehemu nzuri ya kuchoma kuna wengine wanatumia majiko yale ya kuokea nyama wengine wanatumia majiko ya asili.

Unaweza kutumia njia ya kienyeji kwa kuchimba sehemu ambapo unaona hapatakusumbua kuchomea mbuzi wako na akaiva vizuri.


Ukishaandaa jiko lako na mkaa unaweza kuweka nyama yako na kuanza kuchoma.

Utachoma mbuzi wako taratibu kwa moto wa wastani hadi hapo utakapoona ameanza kuiva.

Ukiona ameiva vyema na kuwa tayari kuliwa unaweza kumkatakata vipande na ukamtenga mezani kwa ajili ya kuliwa.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Hii ndiyo nyumba imara

UIMARA wa nyumba ni kuhimili mambo mengi ikiwamo shida zinazojitokeza katika nyakati za mvua, upepo mkali na uzito wowote unaoipiga.

Peter Akoye, anajishughulisha na masuala ya ujenzi wa nyumba, anasema uimara na uzuri wa nyumba unategemea vitu vingi.

Kwamba kwa nyumba za kawaida, uimara wake huanzia kwenye ujenzi wa msingi, kuta, paa, nguzo, mihilimi, milango, madirisha na dari. Haya yanapaswa kuzingatiwa wakati wa ujenzi wake.

"Nyumba imara na mwonekano mzuri ni alama kwa eneo husika, huongeza thamani ya jengo, madhari ya jengo iliyowekwa katika uzuri, pia huleta hisia na utulivu, furaha na uchangamfu kwenye familia na mtaa," anasema Akoye.

"Ni muhimu jengo liwe imara na uzuri unaoendana na matumizi yake, kama ni kwa ajili ya biashara, basi liwe lenye mvuto unaovutia hata wateja, kama ni kwa ajili ya kuishi familia, basi ichangie kuleta amani na furaha nyumbani," anasema.

Anashauri kwamba ni vyema nyumba ikafanyiwa usanifu mzuri na bora kuanzia jengo lenywe, mazingira ya ndani, madhari ya nje ili yabebe maana fulani na kwamba ni muhimu kuwa makini na maana hiyo unayomwambia mtu kupitia nyumba yako.

"Rangi, mpangilio, mpishano, kimo, ukubwa, umbile la nyumba yako huathiri hisia za mtumiaji. Pia niwakumbushe kwamba rangi nyeupe kwenye nyumba huleta hisia za usafi, utaratibu na amani.





"Kijani huleta hisia za utulivu, uasili. Nyekundu huleta hisia za kusisimua, shauku, changamfu.

Rangi ya waridi huleta hisia ya furaha na ya bluu huleta hisia za uasilia na utulivu pia, kwa hiyo ni muhimu kufanya chaguo sahihi unapopanga au unapokamilisha ujenzi wa nyumba ya ndoyo yako," anafafanua.

Anashauri kwamba jambo la msingi ni kujenga nyumba unayohitaji, itakayokidhi mahitaji ya sasa na baadaye, yenye usalama na uimara, iliyo katika uzuri wake na kuepuka kujenga usiyoihitaji.

Kufahamu aina ya nyumba inayokufaa kujenga ni miongoni mwa jambo linalosisitizwa na mtaalamu huyu kwa kuwa ndipo mahali muhimu ambapo kila mtu anapatia faraja na kupata muda wa kupumzika baada ya shughuli nyingi za kujitafutia kipato.

## Jinsi ya kutumia birika ya chai




MAISHA ya kisasa yanakwenda sambamba na wepesi wa kufanya jambo kwa muda mfupi.

Birika la chai la kioo ni chombo kilichotengenezwa kwa ajili ya kumrahisishia mtu kuchemsha chai kwa haraka zaidi kuliko kutumia aina nyingine ya chombo. Kutokana na umuhimu wake, hizi ni baadhi ya njia za kutumia birika la kioo kwa ajili ya kufanya lidumu kwa muda mrefu.

**1:** Usiweke karibu na jiko la gesi, moto au kwenye oveni.

**2:** Usiwashe kama birika halina maji kwa sababu inaweza kuharibu vifaa vya ndani vinavyoruhusu joto.

Ili kulinda dhidi ya moto, mshtuko wa umeme, au jeraha, usitumbukize waya ya umeme, plagi za umeme au kifaa cha kuwekea kwenye maji au vimiminika vingine.

**3:** Daima jihadhari kumimina taratibu maji yanayochemka, weka kwa uangalifu bila kubonyeza kitufe cha mfuniko.


**4:** Ukimaliza hifadhi birika katika eneo kavu na salama.


# KATUNI

## KATUNIKA KI'DOMOKRASIA


BY ABDUL KINGO - 2022
SMS - 0713 447766






*SHOBO - CHANGAMKIA




*KINYUNYIZO CHA LEO...

## JUKWAANI




...SAMAKI HALIWI GIZANI...

## HABARI KIMATAIFA

# Mahakama ya juu Marekani yapiga marufuku wanawake kutoa mimba

**WASHINGTON,** MAREKANI

HUENDA mamilioni ya wanawake nchini Marekani watapoteza haki ya kutoa mimba baada ya Mahakama ya juu zaidi nchini humo kubatilisha sheria iliyopitishwa miaka 50 iliyopita ya utoaji mimba.

Juzi mahakama ya juu zaidi Marekani ilitoa uamuzi wake kwenye kesi iliyofuatiliwa kwa makini na idadi kubwa ya watu wanaotoa mimba

Katika uamuzi wake huo wa kihistoria, mahakama hiyo ilibatilisha haki ya wanawake kutoa mimba nchini humo.

Rais wa Marekani Joe Biden amekosoa vikali uamuzi huo akisema ni 'kosa la kusikitisha lenye athari kubwa'.

Kiongozi huyo alihimiza kufanyika kwa maandamano ya amani miongoni mwa wanaoulaani na kuupinga uamuzi huo, huku akiyarai majimbo kuweka sheria zitakazoruhusu utoaji mimba.

Uamuzi huo umejiri baada ya waraka wa mahakama hiyo kuhusu uavyaji mimba kuvuja kwa vyombo vya habari vya Marekani mapema mwezi Mei.

Rasimu hiyo ilionyesha kuwa Mahakama ya Juu ya Marekani ilikuwa tayari kutengua uamuzi huo wa kihistoria wa Roe v. Wade uliopitishwa mwaka 1973 na ambao uliweka haki ya kutoa mimba.

Nusu ya majimbo yatarajiwa kuweka vikwazo dhidi ya utoaji mimba.

Uamuzi huo unaacha njia wazi kwa uwezekano wa majimbo nchini Marekani kupiga marufuku utoaji mimba.

Saa chache tu baada ya uamuzi huo wenye mtikisiko kutolewa, jimbo la Missouri, lilipiga marufuku utoaji mimba isipokuwa tu kama mimba ilitokana na kisa cha ubakaji au ngono kati ya ndugu wa karibu.

Jimbo la Dakota linatarajiwa kufuata mkondo huo. Gavana wake Kristi Noem, alitoa tarifa akisema uaviaji mimba ni kinyume cha sheria katika jimbo lake, ila tu kama sababu maalum ya kiafya au kimatibabu kuthibisha haja ya mjamzito kuharibu mimba.

Mahakama hiyo ilisema ni wajibu wa kila jimbo kuamua kama litaruhusu uavyaji mimba au la.

"Katiba haijaruhusu haki ya kutoa mimba; uamuzi wa Roe na Casey umebatilishwa na mamlaka ya kusimamia na kudhibiti uaviaji mimba unarudishwa kwa wananchi na wawakilishi wao waliochaguliwa," mahakama hiyo ilisema ikirejelea uamuzi wa mwaka 1992 wa uzazi wa mpango dhidi ya Casey ulioruhusu haki ya utoaji mimba.

**DW**

# Zelensky: Ukraine sio kizuizi Ulaya, Russia

**KYIV,** UKRAINE

RAIS wa Ukraine Volodymyr Zelensky, amepongeza hatua ya nchi yake kupewa hadhi ya kujiunga na Umoja wa Ulaya (EU) na kusema hatua hiyo ni ya mabadiliko makubwa.

Katika hotuba aliyoitoa jana kupitia video, Zelensky alisema kuwa Ukraine sio daraja, sio kizuizi kati ya Magharibi na Russia na sio zuio kati ya bara Ulaya na Asia.

Zelensky aliongeza kuwa nchi yake ni mshirika wa siku za usoni wa takriban mataifa 27 ya umoja huo, na sio taifa la tatu, lakini litakuwa mwanachama wa Umoja wa Ulaya.

Kiongozi wa bunge la nchi hiyo, Ruslan Stefanchuk, alisema kwamba hawawezi kubadili jiografia na kwamba Russia itaendelea kuwa taifa jirani lakini katika hali hii, historia imeishinda jiografia.

**MAKOMBORA 48 YALIPIGA RAIA**

Mshauri mmoja wa kivita, alisema kuwa Russia ilirusha makombora 48 wakati wa usiku wa jana , ambayo yalilenga raia.

"Russia bado inajaribu kuitisha Ukraine, kusababisha hofu na kuwafanya watu waogope, taifa linajua kila kitu, liko tayari kwa lolote na bila shaka itaadhibiwa kwa uovu wote," aliandika Mikhail Podoliak kwenye akaunti yake ya Twitter.

Usiku wa Juni 24 na 25, Russia ilifanya moja ya mashambulizi makubwa zaidi ya makombora huko Ukraine.

**IAEA INA WASIWASI KIWANDA CHA ZAPORIZHZHA**

Shirika la Umoja wa Mataifa la kudhibiti silaha za nyuklia (IAEA) jana lilieleza wasiwasi wake kuhusu wafanyakazi wa Ukraine walioko ndani ya kiwanda cha nyuklia cha Zaporizhzha cha nchi hiyo kinachodhibitiwa na Russia.

Shirika hilo lilisema katika taarifa yake kwamba linafahamu kuhusu ripoti katika vyombo vya habari na kwingineko zinazoashiria hali inayoendelea kudorora kwa wafanyakazi wa Ukraine walioko katika kiwanda hicho kikubwa cha nyuklia barani Ulaya.

Mkurugenzi wa shirika la IAEA Rafael Grossi, alisema hali katika kiwanda hicho haikubaliki huku wafanyakazi hao wako katika mazingira ya shinikizo chini ya udhibiti wa wanajeshi wa Russia.

IAEA imesema lazima ipeleke maofisa wake katika kiwanda hicho haraka iwezekanavyo kulishughulikia suala hilo pamoja na masuala mengine ya dharura.

Mojawapo ya masuala wanayohitaji kuyashughulikia wachunguzi wa IAEA ni kufanya kazi ya uhakiki, ikiwemo kuangalia kiwango kikubwa cha nyenzo za nyuklia katika kiwanda hicho.

**DW**



Dereva akiendesha lori kupita katika kizuizi cha matairi yanayoungua moto mji mkuu wa Quito, baada ya waandamanaji wanaompinga Rais wa Ecuador, Guillermo Lasso, kuendelea kumpa shinikizo la kujiuzulu: **REUTERS**

# Prince Charles ahuzunishwa kuhusu utumwa

**KIGALI,** RWANDA

MRITHI wa kiti cha ufalme nchini Uingereza, Prince Charles, ameelezea huzuni kubwa kuhusiana na utumwa katika hotuba yake kwa viongozi wa nchi za Jumuiya ya Madola wanaokutana nchini Rwanda.

Prince Charles alikiri kwamba misingi ya jumuiya hiyo inatokana na kipindi cha uchungu katika historia.

Wakati wa ufunguzi wa kongamano hilo la siku mbili mjini Kigali, mwanamfalme huyo alisema kuwa hawezi kuelezea ukubwa wa huzuni yake binafsi kuhusu mateso ya watu wengi wakati anapoendelea kuimarisha uelewa wake kuhusu athari za kudumu za utumwa.

Aliongeza kuwa iwapo wataunda mustakabali wa pamoja ambao utawanufaisha wananchi wote, lazima pia watafute mbinu mpya za kutambua maisha ya nyuma na kwamba hayo ni mazungumzo ambayo wakati wake umefika.

Jumuiya ya Madola, yenye nchi 54 zilizokuwa makoloni ya Uingereza, inajumuisha takriban theluthi moja ya binadamu na inajieleza kama mtandao wa washirika sawa, lakini baadhi ya wanachama wamekuwa wakitoa wito wa kuwepo kwa tathmini ya ukoloni huo uliopita

**DW**

MAKALA

# DIPLOMASIA NI MSINGI UTATUZI WA MIGOGORO



Na Magabilo Masambu - 0689157789

**Kama tunavyofahamu Tanzania toka uhuru imeshiriki katika harakati nyingi katika ukanda huu wa Afrika katika kutatua migogoro lakini kushiriki kuzikomboa nchi nyinginezo na kujipatia uhuru wao.**

MNAMO Juni 10, 2022 kupitia taasisi yetu ya vijana Diplomasia yaani Youth Diplomatic Icon (YDI) inayoongozwa na James Leonard Magumba kama Mkurugenzi Mtendaji, tulipata nafasi ya kualikwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia kwa Mwenyekiti wa Bunge, David Mwakiposa Kihenzile. YDI inajihusisha na kutoa mafunzo ya diplomasia ya vijana pamoja na mambo ya itifaki.

Pamoja na kushiriki vikao vya Bunge, tulipata nafasi ya kupata mafunzo kutoka kamati mbalimbali mojawapo ikiwa ni Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Kupitia mafunzo hayo tulipata kufahamu ni kwa namna gani sisi kama taifa tunahusika kutatua migogoro mbalimbali ya ndani, lakini ile inayotuhusu sisi na majirani zetu au migogoro inayotokea nje ya nchi yetu.

Kama tunavyofahamu Tanzania toka uhuru imeshiriki katika harakati nyingi katika ukanda huu wa Afrika katika kutatua migogoro lakini kushiriki kuzikomboa nchi nyinginezo na kujipatia uhuru wao.

Nikiri kwamba Tanzania kama nchi nyingine yoyote duniani, tunazo namna mbalimbali za kuwapata viongozi wetu, wapo wanaochaguliwa au kuteuliwa. Katika kuchaguliwa, yako mambo mbalimbali yanawapa nafasi hiyo, inaweza kuwa ni elimu, fedha ama ushawishi wao.

Kuteuliwa vivyo hivyo kuna mambo mengi yanatazamwa elimu, uzoefu pengine hata uswahiba na pia vinaweza kuwa ni vigezo. Kwa hiyo haimaanishi kwamba mtu yeyote akichaguliwa au kuteuliwa, basi anazo sifa za kuwa kiongozi na kwamba anapoingia ofisini hastahili kupata mafunzo mengine nje ya elimu yake aliyonayo.

Ninachokusudia kusema hapa ni kwamba, diplomasia kama taaluma ambayo inasomwa vyuoni, kuna umuhimu mkubwa kwa viongozi wetu karibu wote kuwa wanapata mafunzo ya mara kwa mara katika eneo hilo na mambo ya Itifaki, hii ni kwa sababu diplomasia ni silaha ya utatuzi wa migogoro pamoja na mambo mengine ya kiutawala hasa uhusiano katika nyanja mbalimbali kama uchumi, siasa, mawasiliano na usalama.

Kiongozi yeyote anapokosa uwezo wa kumaliza mambo yanayojitokeza kwa mazungumzo badala yake akatumia nguvu katika kuyatatua, atakuwa anakosa uhalali wa kuitwa kiongozi badala yake anasalia kuwa mtawala. Hii ni kwa sababu sifa moja kubwa ya kiongozi ni kuwa na uwezo mkubwa wa kushawishi na kufikia makubaliano kwa njia ya mazungumzo, nguvu huwa ni hatua ya mwisho kabisa baada ya juhudi kubwa za mazungumzo kushindwa kukubalika.

Vita vyote vinavyotokea katika mataifa mbalimbali duniani ni ama njia za mazungumzo zimeshindwa kuleta makubaliano au hazifanyiki kabisa na mara nyingi kinachotokea ni kwamba, baada ya kupigana ndipo huwa wanarudi tena kwenye mazungumzo. Unajiuliza kwanini haya mazungumzo yasingefanyika mwanzo na kuokoa maisha ya watu wasio na hatia?

Siku chache tu zimepita tumeshuhudia viongozi wanaounda Jumuiya ya Afrika Mashariki wakikutana jijini Nairobi kujadili hali ya usalama kwenye eneo la mashariki ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ambako DRC na Rwanda zinashtumiana katika mgogoro huo. Wanakutana kufanya mazungumzo hayo, ndiyo tunaita kutatua migogoro kidiplomasia.

Tanzania tukiwa sehemu ya jumuiya hiyo tunawaombea viongozi wetu hawa waweze kufikia makubaliano mema, kwa sababu kakweli ni jambo la aibu sana watu mnajiita mpo kwenye umoja wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, halafu huku mnazozana kila wakati, madhumuni na nia ya kuwa ndani ya umoja inapotea.

Kama yuko anayesababisha migogoro hiyo ndani ya umoja akemewe vikali na hatua za kidiplomasia zichukuliwe ili kutatua migogoro hiyo, kwa sababu wanaoumia ni wananchi wanaoathiriwa na mapigano yasiyoisha hasa kinamama na watoto.

Kwa hiyo, tunaweza kuona jinsi diplomasia ilivyo muhimu katika maendeleo ya kila siku. Hata kwenye ngazi ya familia ni muhimu kupata mafunzo haya, kwa sababu migogoro inayotokea kwenye familia zetu, inasababisha madhara makubwa ikiwamo vifo.

Hatuna uwezo wa kuzuia migogoro, lakini tunatakiwa kutafuta njia bora za kidiplomasia ili kuitatua. Kuna shughuli nyingi sana za maendeleo zinakwama kutokana na baadhi ya viongozi kuwa na uelewa mdogo wa diplomasia ya kiuchumi, wanaendeshwa na ubabe mwisho wa siku wengine wanaharibu mpaka uhusiano na wawekezaji wa ndani na wa nje.

**0689157789**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Dk. Remmy alivyokiimba kifo kuwakilisha mawazo ya wengi



Na Adam Fungamwango

KATI ya wanamuziki walioimba nyimbo nyingi nchini zinazohusiana na mambo ya kifo ni Dk. Remmy Ongalla.

Huyu ni mwanamuziki na mwanafalsafa aliyezaliwa Februari 10, 1947, Kindu, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na kufariki nchini Tanzania Desemba 13, 2010, jina lake kamili likiwa ni Ramadhani Mtoro Ongalla. Remmy ni kifupisho cha jina la Ramadhani.

Aliingia nchini Tanzania mwaka 1978 akiletwa na mjomba wake Mzee Makassy aliyekuwa na bendi yake ya Orchestra Makassy hapa nchini na hii ni baada ya kifo cha Isihaka Gobby aliyeuawa kinyama nchini Tanzania mwaka 1977, wiki mbili zilizopita nilielezea habari zake kwenye safu hii.

Mzee Makassy alikwenda kwao Congo DR (wakati huo ikiitwa Zaire), kutafuta mwanamuziki wa kumrithi Gobby, ndiyo akaangukia mikononi mwa mpwa wake, kwani alimkuta wakati huo ameshaiva kimuziki.

Remmy amefanya mengi sana, lakini leo nataka kumzungumzia, juu ya yeye kuimba nyimbo za kifo.

Ukizisikiliza nyimbo nyingi za mwanamuziki huyo, ni kwamba anaimba kile ambacho binadamu wote wanakifikiria na si kukiongea.

Ukitaka kufahamu hilo, angalia nyimbo za kifo ambazo ameimba, ndiyo utagundua hilo. Hata wanamuziki wenzake wote wa bendi zingine na hata wasanii wa sasa wa bongo fleva, hakuna hata mmoja aliyekielezea kifo kwa mapana na undani wake, ila wakikaa peke yao na kukifikiria wanawaza kama Remmy.

Kukitoa hadharani ndiyo wanashindwa. Hao ni wanamuziki ambao ndiyo kazi yao hiyo, lakini wengi wameshindwa, lakini Remmy ameiweza.

Hakuna binadamu yoyote duniani ambaye hawezi kukaa siku moja hata kwa dakika moja au mbili kukiwaza kifo.

Nitakufa lini? Nitakufa kifo cha aina gani? Wapi? Nitakufa baada ya kina nani kufa? Nitatangulia mimi kabla ya mke wangu? Watoto wangu? Ndugu zangu? na maswali mengi yasiyo na majibu na baada ya hapo mawazo hayo yanaondoka na kuendelea na shughuli zingine mpaka siku nyingine tena litakapokujia wazo hilo. Na bindamu yoyote huwa hapendi kufa ingawa anajua kipo, au kama ikiwezekana awe wa mwisho yeye.

Haya huwa ni mawazo ya kimya kimya tu, si rahisi kumuona mtu akikaa na wenzake, ndugu jamaa, marafiki, mkewe na kuwaambia au kuwauliza maswali kama hayo, anaweza kuonekana na matatizo kichwani.

Ila kwa wanamuziki na wasanii huo ndiyo wajibu wao kuwakumbusha binadamu kuna siku ya kuzaliwa na ya kufa, lakini kazi hiyo akaifanya Dk Remmy.

Tunaanza na wimbo wa 'Siku ya Kufa' alioupiga akiwa na bendi ya Orchestra Makassy, mara tu baada ya kujiunga.

"Siku ya kufa wandugu kwa heri, siku ya kufa nyama ya udongo, uzuri wote unaoza, ujana wote unakwisha, akili yote inakwenda, nyumbaa uliyoijenga inabaki, watoto uliowazaa wanalia, maiti haina rafiki, marafiki zangu watanikimbia. Tulikuwa tunakula pamoja, tulikuwa tunakunywa pamoja, wanakuwa wanishangaa, wanakuwa wananiogopa, nakuwa leo shetani."

Hajabakisha kitu, ni kweli mtu anapokufa anakwenda kuzikwa, nyama yake inakuwa udongoni, hata kama ulikuwa mzuri na mrembo vipi, ukishazikwa mwisho wake ni kuoza tu. Ujana wote unakwisha na hata kama ulikuwa mjanja vipi, kwisha habari yako. Hakuna kilichobaki, kwani hata watoto wako, mke, mume, hawatokuwa na msaada wowote kwako zaidi ya kukulilia. Ni kweli maiti haina rafiki kwani hata mkeo au mumeo ambaye ulilala naye chumba kimoja, kitanda kimoja, akifa hata uambiwe ulale naye tu chumbani kwa usiku mmoja, hutoweza.

Marafiki watakukimbia, ni kweli kwa sababu hata wanapoaga maiti, inaonyesha kuwa si rafiki tena, na wakishatoka makaburini, kila mtu na lake tena, wamekuacha, maisha yanaendelea.

"Siku ya kufa wandugu wandugu kwa heri, siku ya kufa nyama ya udongo, siku ya kufa utalala unaoza, siku ya kufa utakwenda na nani? Dar es Salaam kwa heri, Tanzania kwa heri."

Hapa Remmy anauliza, siku ya kufa utakwenda na nani? Ukweli ni kwamba kila mtu anakufa kwa siku yake, hakuna anayekwenda na mtu yoyote hata kama awe mumeo, mkeo, rafiki ambao mlikuwa mnapendana sana, hamtakufa au kuzikwa pamoja.

Kuna wimbo wa 'Kifo Hakina Huruma', ambao aliupiga na Super Matimila. Baadhi ya mashairi yake ni haya. "Kifo kwa nini hakionekani, kifo umejificha wapi? Kifo ungekuwa unaonekana tungekupa rushwa kusudi tuishi milele.

Siku yangu ikifika, niarifu mapema, niage ndugu zangu, watoto zangu, pesa zangu nizitawanye, zilizobaki nizile mwenyewe...kifo hajui uzuri wako, kifo hajali cheo chako, umwamba wako. Kifo ni kiboko yao .

Remmy anawakilisha mawazo ya wengi wanaojiuliza hivi kifo ni nini? Kimejificha wapi? Na kwa nini hakionekani? Na ni kweli kabisa kingeonekana nadhani ni masikini tu ambao wangekuwa wanakufa mapema, kwa sababu wangetoa rushwa na pesa zingewaishia, wangebaki matajiri ambao wangeishi maisha marefu. Kifo hajali chochote, uzuri, cheo, ubondia, utemi, wala nini, na wala hakichagui, anaweza kufa mzima, akabaki mgonjwa"

Wimbo wa 'Siku Yangu Ikifika' ambao uliuimba tena na Super Matimila, anazidi kujiuliza na kusema

"Nitalala peke yangu jeneza langu peke yangu, sanduku langu peke yangu, kwenye kaburi milele na milele, hamtaniona tena."

Binadamu akizikwa kinachobaki ni historia tu. Mwili wake utalala humo daima.

"Kwa Mungu kuna nini? Mbona walioondoka hawarudi kutuambia? Waliotangulia ni kimya. Kwa nini udongo kwa nini hushibi? Unatumaliza kila leo. Binadamu akila akishiba anaacha kula, lakini udongo ardhi haushibi na unakula watu kila siku.

Maiti haina thamani, unaweza kuzikwa kwenye matope, hausemi, kifo na mfungwa sawa sawa. Ukifa kila kitu kimekufa." Ni maneno mazito kwenye wimbo huo ambayo kila binadamu huwa anajiuliza kimoyomoyo. Lakini Remmy ameyatoa hadharani na kuimba kwa hisia.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

PRINCE Petit kijana aliyelelewa kwenye mazingira ya ajabu. Amelelewa na baba yake mzazi tu bila mama. Madada wa kazi waliopewa kazi ya kumlea walipewa mkataba wa mwaka mmoja mmoja tu na wanapomaliza hawakuongezwa. Hakupelekwa shule yoyote ile, badala yake walimu walilipwa pesa kwa ajili ya kumfundisha nyumbani tu. Hata alipokuwa akipata nafasi ya kwenda kufurahia maisha na kuitazama dunia nje ya nyumba yao, alipewa angalizo la kutozoena na mtu yeyote yule. Aliingiziwa falsafa na vitu vingine kichwani mwake mpaka akawa na tabia ambazo ni tofauti na umri wake. Akiwa na miaka mitano tu, alianza kufundishwa kulenga shabaha na alipofikia miaka minane tu alikuwa na uwezo wa kutumia bastola ya aina yoyote ile na angeweza kuajiriwa kwenye shirika lolote la kijasusi duniani Anapofika umri wa miaka 25, baba yake mzee Pokwa anamtuma kazi. Kazi ya kuua na kulipiza kisasi. Ni kwa nini? Anakwenda kumuua nani? Kwa nini baba anayejua mkasa mzima asiende mwenyewe? Kitu gani kilichotokea huko nyuma? Nakala yako ya Nipashe itakufanya kujua kilichopo nyuma ya pazia.

# Mwisho wa Mauaji-7

**Na Adam Fungamwangwo (0716 350534)**

NI dakika 15 tu zilizofuata macho yake yalimuona mtu mmoja aliyekuwa amevaa kanzu, mkononi akiwa na mkoba.

Wala hakutaka kujiuliza mara mbili kuwa alikuwa ni mzee Hussein. Alilielekea gari ambalo lilikuwa pale. Alipofika kwenye mlango ni kama alizubaa kidogo, aliangalia alikotoka na kuchelewa kufungua mlango wa gari kwa ufunguo aliokuwa nao.

Prince alikiona vizuri kichogo cha mzee Hussein vizuri mno pale alipokuwa akiangalia mlangoni. Ni kweli alikuwa akimuangalia kijana mmoja ambaye alikuwa anatoka na kusimama mlangoni, nadhani kwa sababu za kiusalama zaidi.


Ni hapo hapo alipokuwa anapahitaji. Hakuwa na muda mwingine tena. Ni risasi moja tu iliyokwenda kupenya kwenye kichogo cha mzee Hussein na kutokea mbele kwenye paji la uso. Ilimrusha pia hatua kadhaa mbele na mkoba wake.

Kwa sababu hakuwa na shida ya mkoba, Prince alichofanya ni kugeuka tu na kuondoka, huku yule kijana aliyekuwa mlangoni akitoa bastola yake na kuanza kupiga hovyo akidhani kuwa ni majambazi wamevamia kwa lengo la kumpora pesa zake. Hakuona mtu yoyote akijitokeza kuja kuokota mkoba ule, lakini hakujiamini akaendelea kumimina risasi zilizowafanya watu wengi waliokuwa eneo jirani kutimua mbio.

Kilichoendelea hapo ni kwamba askari polisi baada ya kufika waliambiwa kuwa majambazi walivamia kwa lengo la kutaka kumpora pesa mzee Hussein. Walichofanikiwa ni kutoa uhai wake, lakini kijana yule alipambana sana na majambazi ambao walikuwa wengi, lakini kijana yule alipambana nao sana na kushindwa kuchukua pesa.

Kijana yule alionekana shujaa. Japo mzee Hussein aliuawa, lakini alifanikiwa kuwadhibiti kiasi cha kushindwa kufanikisha azma yao ya uporaji.

Wala hakupata tabu sana kuondoka eneo la tukio, milio kadhaa ya risasi iliyofuatia baada ya yeye kupiga risasi moja tu na kumuondoa uhai mzee Hussein, ilimfanya kuondoka kwa usalama zaidi kwani watu wengi eneo la Manzese Argentina walikuwa wakikimbizana, kila mmoja kuokoa uhai wake.




**"Sasa wamebaki watatu. Ukiwamaliza hao utakuwa umemaliza kila kitu. Nadhiri yangu niliyoweka kwenye kaburi la mama yako kuwa nitawamaliza wote waliodhulumu mali zako na uhai wako. Leo mwanangu unaniheshimisha kwa kufanya kile nilichokusudia, kukufundisha kulipa kisasi cha mama yako.**

Nusura acheke, kwani wengine walikuwa kwenye eneo la tukio na kukimbilia sehemu zingine, lakini wengine walikuwa wakitoka maeneo yenye usalama na kukimbilia eneo la tukio bila kujua.

Ni kwa sababu hakuna aliyekuwa akijua kwa usahihi ni wapi hasa risasi zilikuwa zinamiminwa.

Aliona baadhi ya abiria wakishusha ndani ya daladala, wengine kuruka madirishani na kila mmoja kutimua na njia yake. Wapo pia waliokuwa nje na mirindimo ya risasi iliwafanya kurukia daladala ambako waliona ni sehemu salama kuliko chini.

Ni yeye pekee ndiye alikuwa anajua kwa usahihi ni wapi risasi zilipigwa.

******************************

"Unafanya kazi nzuri sana kijana wangu. Mpaka sasa hakuna sehemu yoyote ile uliyokosea, kushindwa kutekeleza nilivyokutuma na kikubwa zaidi ni kwamba mpaka sasa polisi hawajui ni nani anafanya haya yote.

Hawajui kama muuaji wa mzee Sabri ndiye muuaji wa mzee Hussein ni mmoja. Wanasema eti wanaendelea kumsaka muuaji wa Sabri ambaye bado hawajampata, lakini wanaendelea kumtafuta aliyemuua mzee Hussein." Mzee Pokwa aliongea kwa sauti nzito na ya chini, lakini yenye furaha.

"Ahsante baba." Akajibu Prince kwa sauti ya kibabe iliyochanganyikana na maringo.

Tayari alishaanza kuonekana kuzoea kazi hiyo, na hata woga ulishaanza kumuisha. Kwanza kabisa ni kwa sababu kila anapotekeleza mauaji anayafanya kwa ustadi wa hali ya juu kiasi kwamba inakuwa haimpi shida kufanya kwa wakati na kuondoka eneo la tukio bila kushtukiwa. Pili amekuwa haachi hata chembe ya ushahidi ambayo inaweza kuwapa askari pa kuanzia ushahidi na kuwapeleka kwa muuaji mwenyewe.

Tatu, alijawa na ujasiri na hasira kutokana na kila anapokumbuka kuwa watu hao ndiyo walimuua mama yake mzazi baada ya kumdhulumu shamba. Nne pia alijua ni hao hao ndiyo waliokuwa wanamsaka akiwa mdogo ili wammalize.

"Sasa wamebaki watatu. Ukiwamaliza hao utakuwa umemaliza kila kitu. Nadhiri yangu niliyoweka kwenye kaburi la mama yako kuwa nitawamaliza wote waliodhulumu mali zako na uhai wako. Leo mwanangu unaniheshimisha kwa kufanya kile nilichokusudia, kukufundisha kulipa kisasi cha mama yako. Tukishamaliza mtu wa mwisho, nitakupeleka kwenye kaburi lake kwenda kutambika na kumueleza kuwa tumemaliza operesheni baada ya miaka mingi na yeye apumzike kwa amani." Aliongea na kuonekana na furaha sana.

"Watatu hao ni wapi na lini nikamilishe kazi hiyo? Akauliza Prince. Akakohoa kikohozi chepesi na kuendelea. "Mimi nataka nikamilishe hiyo kazi mapema, ili sasa nikae kwa amani."

"Ni kweli mwanangu unatakiwa kukamilisha mipango hii ili uishi bila mikiki mikiki tena. Najua ukimaliza hutofanya kazi hii tena ya kuua maisha yako yote. Labda kitokee tena kitu kama hiki kilichompata mama yako, kwa sababu maisha ni safari ndefu sana." Mzee Pokwa alipomaliza kuongea maneno haya, ananyanyuka na kuingia chumbani kwake.

Dakika moja iliyofuatia alirejea akiwa na picha mbili. Akampatia kijana wake.

"Hiyo picha namba moja ni ya jamaa mmoja anaitwa Nassor, na hiyo namba mbili ni Nasir. Hawa ni mapacha. Nao pia wameshiriki mauaji ya mama yako mzazi, hawatakiwi kuishi."

Baada ya kuongea hivyo alimtazama kijana wake halafu akaendelea.

"Taarifa za udukuzi nilizozipata leo mchana ni kwamba kesho jioni watakuwa kwenye harusi maeneo ya Tuangoma, Kigamboni.

Nasema hivi kwa sababu kama utachanga karata zako vizuri, unaweza kuwamaliza wote wawili kwa wakati mmoja. Ni kwa sababu watakuwa kwenye gari moja." "Du, baba hizi taarifa zao huwa unazipataje?" Prince akashangaa.

"Nina vyanzo vyangu mimi, ingawa havijui kuwa nataka kujua habari zao kwa sababu ya kuwamaliza."

**ITAENDELEA JUMAPILI**




# Diamond akifa bendera je?

STAA wa muziki wa kizazi kipya nchini Tanzania, Diamond Platnumz ametoa mpya. Siyo ngoma, hapana. Ameposti kwenye insta stori yake maneno yafuatayo.

"Kiufupi ikitokea nimekufa bendera (Akaweka picha ya nembo ya bendera ya Tanzania ) haipo hapo pengine top 100 Insha Allah."

Ina maana anatuambia kuwa ikitokea mapenzi ya Mungu yeye akatangulia mbele ya haki, basi bendera ya Tanzania haitapeperuka au muziki wa Bongo hautokuwepo hata kumi bora ya muziki Afrika na dunia kwa ujumla.

Amelazimika kuandika haya baada ya kutajwa na kuwa ni miongoni mwa wasanii 10 kutoka Afrika wenye ushawishi mkubwa duniani na mtandao mmoja.

Diamond ameshika nafasi ya nne kwenye 10 bora hiyo, ambayo inaongozwa na wasanii wawili, Wizkidayo na Burna Boy.

Wengine ni Davido aliyeshika nafasi ya pili, Okay Yo namba tatu, Diamond wa nne, Kizz Daniel, Koffi Olomode, Fireboy DML, Heisrema, Fally Ipupa na Temsbaby.

Ujumbe huu unaonekana kuueleza umma kuwa yeye ndiye aliyebaki anaiwakilisha vema nchi linapokuja suala la kimataifa kwa sasa.

# Mocco sasa kaingia mwenyewe

MTAYARISHAJI wa muziki Mocco, baada ya kufanya kazi hiyo kwa muda mrefu, sasa kaona msinitanie, ngoja niingie mwenyewe kwenye fani hiyo.

Ameamua kuingia kwenye fani ya kuimba, baada ya miaka sita ya kuwatayarishia wenzake muziki, mabiti, vinanda na kila kitu.

"Nikiwa kama prodyuza imekuwa safari nzuri sana kwenye maisha yangu namshukuru sana Mungu kwa kila hatua pia nawashukuru sana wote mnaopokea kazi zangu nakuzisapoti

Lakini pia nilikuwa natamani siku moja watu wasikie upande wa pili wa talanta yangu nyingine, hapa nazungumzia upande wa uimbaji kwani ilikuwa ndoto yangu ya muda mrefu sana, hivyo basi ninafuraha kubwa sana kuwakaribisha mashabiki na wadau wa muziki nitawaletea wimbo wangu wa kwanza ambao utapatikana kwenye majukwaa yote ya mitandao ya kijamii duniani."

Ngoma yake ambayo hakuitaja jina alianza kuiachia tangu Ijumaa kwenye mitandao mbalimbali ya kijamii.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### JESUS NA ARSENAL

ARSENAL wamefikia makubaliano ya kumnunua mshambuliaji wa Manchester City na Brazil, Gabriel Jesus kwa pauni milioni 45 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25. ***(Fabrizio Romano)***

### WIJNALDUM KURUHUSIWA

KIUNGO wa kati wa Uholanzi, Georginio Wijnaldum ataruhusiwa kuondoka Paris St-Germain msimu huu wa joto. Leicester City wanamtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, wakati Everton, Wolves na West Ham pia wanafuatilia kwa karibu hali hiyo. ***(90min)***

### TUCHEL KUSAJILI SITA

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel ameahidiwa kusajiliwa wachezaji sita msimu huu na wamiliki wapya wa klabu hiyo. ***(Telegraph)***

### BAYERN YAMKATAA RONALDO

MKURUGENZI wa Bayern Munich, Hasan Salihamidzic amesema hakuna ukweli katika uvumi kwamba, klabu hiyo ya Ligi Ujerumani, Bundesliga, inataka kumsajili mshambuliaji wa Manchester United na Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37. ***(Sky Germany)***

### RAPHINHA AITAKA BARCA

KLABU ya Leeds United na winga wa Brazil, Raphinha mwenye uimri wa miaka 25, amekataa ofa kutoka kwa Klabu za Ligi Kuu England kwa sababu anataka kujiunga na Barcelona. ***(Sport)***

### KEPA KUUZWA

CHELSEA itasikiliza ofa kwa mlinda mlango wa Hispania, Kepa Arrizabalaga baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 kuiambia Marca kwamba "lengo lake wazi ni kucheza." ***(Mirror)***

### RANGNICK NA MAN

MANCHESTER United na Ralf Rangnick walikubali kukatisha uhusiano mwishoni mwa msimu uliopita kwa kiasi fulani kwa sababu ya kocha, Erik ten Hag kusita kufanya kazi na Mjerumani huyo katika jukumu lake la ushauri lililopendekezwa. ***(ESPN)***

### LENGLET ATAKIWA

BARCELONA wanatumaini Tottenham Hotspur inaweza kumshawishi mlinzi wa kati wa Ufaransa, Clement Lenglet mwenye umri wa miaka 27, kuhamia Ligi Kuu England. ***(ESPN)***

### SPENCE BADO

KLABU ya Tottenham na Middlesbrough bado hazijaafikiana kuhusu ada ya uhamisho wa beki wa kulia wa timu ya taifa ya England, chini ya umri wa miaka 21 Djed Spence. ***(Sun)***

### ANTHONY KUMFUATA HAG

WINGA wa Brazil, Anthony mwenye umri wa miaka 22- ambaye ana nia ya kuungana na kocha wa za zamani Erik ten Hag kule Manchester United - alikosekana wakati Ajax iliporejea mazoezi ya kujiandaa na msimu Ijumaa. ***(Mirror)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# GABRIEL JESUS RASMI KUTUA ARSENAL

●●● Atakuwa mchezaji anayelipwa mshahara mkubwa zaidi hapo Emirates huku...

**LONDON,** England

ARSENAL wamefikia makubaliano na Manchester City kumsajili mshambuliaji wa Brazil, Gabriel Jesus, kwa mujibu wa 90min.

**Makubaliano kati ya klabu hizo mbili yalikamilishwa Ijumaa jioni, na thamani ya uhamisho ikiwekwa karibu pauni milioni 45.**

Na sasa Jesus anatarajiwa kwenda London Kaskazini kwa ajili ya vipimo vya afya huku wawakilishi wake wakifanua kuhusu maslahi yake binafsi.

Hayo yalikuwa tayari yanajadiliwa na yanatarajiwa kukamilishwa wiki hii, huku Jesus akitarajiwa kuwa mchezaji anayelipwa zaidi Arsenal - akilipwa zaidi ya pauni 250,000 kwa wiki.

City walikuwa na matumaini wangeweza kumshawishi Jesus kubaki na ofa yao ya mkataba mpya haikuwa mbali na kile anachotarajia kupata kule kwenye Uwanja wa Emirates.

Lakini mabingwa hao wa Ligi Kuu England walikuwa wamemweleza wazi Jesus kwamba, wangemuuza msimu huu wa joto ikiwa hatakubali mkataba mpya, na hilo limetimia sasa Arsenal wamefikia thamani yao.

Vyanzo vya karibu na Jesus vimethibitisha kwamba Mbrazil huyo alikuwa na nia ya kutumia 'nafasi mpya' Arsenal na hiyo ikiwa ni pamoja na kucheza nafasi muhimu.

Kocha wa City, Pep Guardiola alimchezesha Jesus pekee kama mshambuliaji wa kulia katika kipindi cha miaka miwili iliyopita na Mhispania huyo hakuwa na mpango wa kubadilisha.

Erling Haaland amesajiliwa kutoka Borussia Dortmund msimu huu wa joto na kuwa mshambuliaji chaguo la kwanza wa klabu hiyo.

Hilo linafahamika kuwa lilikuwa na mchango mkubwa kwa Jesus kuamua kuondoka.

Arsenal wamewazidi kete Chelsea, Tottenham Hotspur, AC Milan, Juventus na Atletico Madrid ambazo zilikuwa zikimtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25.

## HABARI BURUDANI

SportPesa
LIVE IN PLAY

MECHI KALI
MISR LEL MAKASA
VERSUS
AL MASRY CLUB
1 | 4.01
X | 3.06
2 | 2.01

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa




# ROONEY AACHANA NA DERBY COUNTY

**LONDON,** England

KLABU ya Derby County imetangaza kuachana na kocha wao, Wayne Rooney baada ya yeye mwenyewe kuomba kuondoka.

Matatizo ya kifedha ya Derby yameidhoofisha klabu hiyo kwa misimu michache iliyopita na waliambulia pointi 21 wakati wa msimu wa 2021/22, na walishuka daraja kutoka championship hadi League One.


Klabu hiyo ilitangaza Ijumaa jioni kwamba, Rooney ameondoka kwenye klabu hiyo.

Taarifa kutoka kwa wasimamizi wa pamoja wa Derby ilisema: "Wasimamizi wa pamoja wamesikitishwa sana na Wayne kuchukua uamuzi mgumu wa kuondoka klabuni na tumetumia muda leo kumshawishi abaki, lakini imeshindikana.

"Tunamshukuru sana kwa kazi nzuri aliyoifanya licha ya hali ngumu ya uwanjani msimu wa 2021/22 na tunavutiwa na jinsi alivyoiongoza timu, klabu na jamii katika masuala mbalimbali ya nje ya uwanja."

Katika maelezo yake mwenyewe, Rooney aliweka wazi sababu za kuondoka kwake.

"Katika kipindi cha joto nimekuwa nikifuatilia kwa karibu maendeleo kuhusu umiliki wa Derby County," alisema.



## *Kepa ataka zaidi Chelsea*

**LONDON,** England

KEPA Arrizabalaga anaamini uchezaji wake katika muda mchache wa mechi akiwa Chelsea utahitaji dakika zaidi anapofikiria mustakabali wake katika klabu hiyo.

Kipa huyo alisajiliwa kwa kitita cha pauni milioni 72 mwaka 2018, na alioonekana kuwa chaguo namba moja pale Stamford Bridge.

Edouard Mendy alisajiliwa ili kutoa ushindani kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania, Oktoba 2020, lakini alichukua nafasi ya Kepa kama kipa chaguo la kwanza.

Dakika za Kepa kucheza tangu wakati huo zilipungua, kwani alipata nafasi tu wakati Mendy alipokuwa kwenye michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika, Januari.

Huku mchezaji mwenzake huyo akiwa hana uwezekano wa kuondolewa kwenye kikosi cha kwanza, Kepa anaweza kuondoka Chelsea msimu huu wa joto na tayari amekuwa akihusishwa na klabu kadhaa barani Ulaya - haswa Lazio.

Akizungumzia mustakabali wake katika mahojiano na Marca, Kepa alisema: "Nina furaha, ninatamani, nina hamu ya kuanza, kujifurahisha na, zaidi ya yote, kucheza zaidi. Nataka kuwa uwanjani kwa michezo zaidi.

CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

# BONDIA MFAUME ATAMBA KUMCHAPA MMISRI

Na Saada Akida

BONDIA wa ngumi za kulipwa, Mfaume Mfaume amesema amejiandaa vizuri kupeperusha bendera ya Tanzania dhidi ya, Abdumonem Said wa Misri katika pambano la ubingwa wa kuwania mkanda wa WBF.

**Pambano hili linatarajiwa kuchezwa Julai Mosi ya mwaka huu katika ukumbi wa Diamond Jubilee, Dar es Salaam.**

Akizungumza na gazeti hili Mfaume alisema maandalizi yanaendelea vizuri kwa sababu ya kuhakikisha analipa heshima Taifa lake kwa kumpiga mpinzani wake mapema..

"Nimejiandaa vizuri dhidi ya Abdumonem, nimemfuatilia ni mzuri, naendelea kufanyia kazi ubora wa mpinzani wangu nina imani kwa maandalizi ninayopata nitafanya vizuri na pambano hilo litarejesha heshima yangu," alisema Mfaume.

Alisema amepata muda wa kujiandaa na kufanikiwa kufanyia kazi mbinu zake ili kuwa bora zaidi na kuleta heshima kwa taifa.

Katika pambano hilo kutakuwa na michezo ya utangulizi ambayo Laurent Sengu dhidi ya Thomas Eugen, Pius Mpenda atazichapa na George Dimoso na Oscar Richard dhidi ya Bongani Makovora.

Pambano lingine la utangulizi litakuwa kati ya Juma Choki dhidi ya Issa Nampepecha, Hamis Maya atavaana na Murdoche Katembo na Ibrahim Class dhidi ya Peter Pembeni.





Mke wa Rais wa Zanzibar, Mariam Mwinyi (katikati) akiongoza mazoezi baada ya kutembea kutoka barabara ya ofisi ya Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) Mazizini hadi Uwanja wa Amaan, ikiwa ni ahadi yake ya kushirikiana na Wananchi kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi kufanya mazoezi. **PICHA: IKULU**

# Simba Queens kushusha vifaa vipya

Na Saada Akida

KOCHA Mkuu wa Simba Queens, Sebastian Nkoma amesema usajili unaendelea na watashusha mashine tatu za hatari kutoka nje ya nchi kwa ajili ya kuimarisha kikosi chao kuelekea michuano ya Ligi ya Mabingwa kwa Wanawake ukanda wa CECAFA, yanayotarajia kufanyika Agosti mwaka huu, Arusha.

Hadi sasa Simba Queens imetambulisha wachezaji wapya wawili akiwemo kiungo mkabaji kutoka klabu ya Gaspo FC ya Kenya, Vivian Corozone Aquino na Zainabu Ally wa timu ya Baobab Queens ya Dodoma.

Nkoma amesema wanaendelea na usajili kwa kuimarisha baadhi ya nafasi ikiwemo safu ya ushambuliaji huku wakitarajia kusajili mchezaji kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Alisema kwa sasa hawezi kuweka wazi jina la mchezaji huyo kwa sababu utaratibu wa usajili unaendelea na baada ya kukamilika wataweka wazi majina yao.

"Bado usajili unaendelea kwa kuimarisha kikosi changu, tunahitaji kufanya vizuri katika michuano ya ukanda wa CECAFA na kupata nafasi ya kwenda kuwakilisha nchini katika mashindano ya Mabingwa kwa wanawake," alisema Nkoma.

Alisema wanafanya usajili kwa nafasi ambazo zimekuwa na mapungufu makubwa na kuboresha kikosi chao kwa ajili ya kufanya vizuri kwa msimu mpya wa mashindano.

Kocha huyo alisema wamedhamiria kufanya kweli katika mashindano ya CECAFA baada ya msimu uliopita kuishia katika hatua za awali na mwaka huu wanahitaji kufika mbali kwa kwenda kuwakilisha Tanzania katika michuano ya Afrika.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 26/06/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1413 | Pohang Steelers vs Sangju Sangmu | 2.01 | 3.28 | 3.38 |
| 13:00 | 2300 | Renofa Yamaguchi vs Ventforet Kofu | 3.73 | 3.24 | 1.91 |
| 13:00 | 4055 | Omiya Ardija vs Zwiegen Kanazawa | 2.65 | 3.09 | 2.50 |
| 13:00 | 5764 | Sagan Tosu vs FC Tokyo | 2.21 | 3.04 | 3.14 |
| 13:30 | 5416 | Gangwon vs Jeju Utd | 3.23 | 3.19 | 2.10 |
| 14:00 | 1857 | Utsiktens BK vs IK Brage | 2.28 | 3.52 | 2.96 |
| 14:00 | 2921 | Motala Aif vs Piteaa IF | 2.05 | 3.77 | 2.89 |
| 14:00 | 3363 | Gwangju vs Gyeongnam | 1.83 | 3.53 | 3.68 |
| 14:00 | 5627 | Daejeon Citizen vs Gimpo Citizen | 1.64 | 3.64 | 4.62 |
| 14:00 | 5902 | Skovde Aik vs Vasteras SK | 2.69 | 3.51 | 2.48 |
| 14:30 | 1477 | Chengdu Qianbao vs Shenzhen | 2.89 | 3.09 | 2.32 |
| 15:00 | 3660 | Sandvikens IF vs Umeaa FC | 1.54 | 4.21 | 4.70 |
| 16:00 | 1545 | Dalkurd FF vs AFC Eskilstuna | 2.79 | 3.66 | 2.34 |
| 16:00 | 2200 | Degerfors vs AIK Football | 5.12 | 4.14 | 1.51 |
| 16:00 | 2625 | Hammarby vs BK Hacken | 1.90 | 3.53 | 3.43 |
| 16:00 | 3694 | FC Minsk vs Belshina | 1.62 | 3.62 | 4.80 |
| 16:00 | 4359 | Stabaek vs Fredrikstad | 1.58 | 3.87 | 4.80 |
| 16:00 | 4943 | Raufoss vs Skeid Fotball | 1.71 | 3.77 | 4.02 |
| 16:00 | 5176 | Mjallby vs Norrkoping | 3.34 | 3.14 | 2.07 |
| 16:00 | 5739 | IK Start vs Kongsvinger IL | 1.41 | 4.53 | 5.91 |
| 18:00 | 2904 | Dinamo Brest vs Dinamo Minsk | 6.68 | 4.03 | 1.42 |
| 18:00 | 4049 | Tegs SK vs Sollentuna Utd FF | 6.86 | 4.90 | 1.33 |
| 18:00 | 5933 | Belgium W vs Austria W | 2.70 | 3.29 | 2.35 |
| 18:30 | 3051 | GIF Sundsvall vs Djurgardens IF | 6.67 | 4.61 | 1.36 |
| 19:00 | 1771 | Ham-Kam vs Sarpsborg | 2.62 | 3.38 | 2.52 |
| 19:00 | 4204 | Sandefjord vs Tromso | 3.06 | 3.31 | 2.24 |
| 19:00 | 4293 | Molde vs Jerv | 1.16 | 7.22 | 13.04 |
| 19:00 | 5171 | San Lorenzo vs CA Tigre | 2.90 | 3.09 | 2.32 |
| 19:00 | 5273 | Stromsgodset vs Lillestrom | 2.67 | 3.43 | 2.44 |
| 19:00 | 5777 | Bodo Glimt vs Aalesunds | 1.38 | 5.01 | 6.61 |
| 19:30 | 5853 | Antofagasta vs Deportes Limache | 1.27 | 5.11 | 8.65 |
| 20:00 | 2772 | FK Arsenal Dzerzhinsk vs Slavia Mozyr | 3.15 | 3.35 | 2.07 |
| 20:00 | 5222 | Misr Lel Makasa vs Al Masry Club | 4.01 | 3.06 | 2.01 |
| 21:00 | 3043 | FC Carlos Stein vs Club Cienciano | 3.64 | 3.49 | 1.86 |
| 21:00 | 3507 | Club Almagro vs Deportivo Riestra | 1.97 | 2.95 | 3.93 |
| 21:00 | 4470 | Deportivo Madryn vs Almirante Brown | 2.05 | 3.04 | 3.53 |
| 21:00 | 4562 | Valerenga vs Odd Ballklubb | 1.68 | 3.87 | 4.52 |
| 21:30 | 5891 | Deportivo Maipu vs All Boys | 1.97 | 3.04 | 3.78 |
| 22:00 | 1885 | Agropecuario vs Santamarina | 1.62 | 3.39 | 5.31 |
| 22:00 | 3425 | Avai vs Palmeiras | 5.29 | 3.67 | 1.57 |
| 22:00 | 4104 | Botafogo RJ vs Fluminense | 2.50 | 2.99 | 2.74 |
| 22:00 | 4307 | CD Palestino vs Cobreloa | 1.55 | 3.77 | 5.29 |
| 22:00 | 4631 | Santiago Wanderers vs Curico Unido | 3.24 | 3.39 | 2.01 |
| 22:00 | 5076 | Los Angeles FC vs NY Red Bulls | 1.89 | 3.76 | 3.76 |
| 22:00 | 5558 | Estudiantes Rio Cuarto vs Villa Dalmine | 2.01 | 3.00 | 3.74 |
| 22:00 | 5863 | Mitre SdE vs San Martin SJ | 2.43 | 3.03 | 2.79 |
| 22:30 | 5815 | Independiente Rivadavia vs San Telmo | 1.66 | 3.53 | 4.70 |
| 23:00 | 5578 | Ferroviario CE vs Floresta CE | 2.10 | 2.94 | 3.52 |
| 23:30 | 1225 | Sport Huancayo vs Universitario | 1.54 | 3.89 | 5.12 |
| 23:30 | 4160 | Olimpia Asuncion vs 12 de Octubre de Itaugua | 1.48 | 3.94 | 5.91 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumapili Juni 26, 2022

Nipashe




Jesus rasmi kutua Arsenal UKURASA 21




Nahodha wa Yanga, Bakari Mwamnyeto akiwa ameinua kombe la Ligi Kuu Tanzania bara juu akishangilia na wachezaji wenzake, mara baada ya kukabidhiwa jana kwenye uwanja wa Sokoine, Mbeya. **PICHA: YANGA**

# Yanga yafunika Mbeya

**Na Adam Fungamwango**

## ●●● Yakabidhiwa rasmi kombe lake ikilazimishwa sare, sherehe kuendelea leo Dar es Salaam...

ILIKUWA ni saa 12:07 jioni kwa saa za Afrika Mashariki wakati nahodha wa Yanga, Bakari Mwamnyeto alipolipokea kombe la ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara jana kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, kwenye mikono ya mgeni rasmi Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Innocent Bashungwa.

**Ilikuwa ni baada ya mechi ya raundi ya 29 dhidi ya Mbeya City jana jioni, timu hizo zikitoka sare ya bao 1-1, ikishuhudia Yanga ikitwaa ubingwa huo mara ya kwanza baada ya misimu minne.**

Ni mara ya kwanza kwa mchezaji huyo kupokea kombe hilo tangu aanze karia yake ya soka, lakini pia anaingia kwenye rekodi ya manahodha wa timu hiyo walioopokea kombe la ubingwa huo, ikiwa ni mara ya 28 sasa.

Deus Kaseke ndiyo mchezaji pekee ambaye alikuwepo wakati Yanga ikitwaa ubingwa kwa mara ya mwisho, wakati huo nahodha akiwa ni Nadir Haroub 'Cannavaro'.

Kwenye mechi hiyo, Yanga haikuonekana kuwa kwenye ubora wake uliozoeleka.

Hata hivyo, bado Yanga imeweza kulinda rekodi yake ya kutopoteza mechi yoyote ile kwenye mechi ya jana, ikibakisha mechi moja tu itakayocheza Jumatano ijayo dhidi ya Mtibwa Sugar, Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Dakika ya saba Makambo aliwakosakosa Mbeya City, aliyemegewa pande na Yassin Mustapha, lakini shuti lake lilimbabatiza kipa Haroun Mandanda na mpira ukaenda juu.

Wakati uko juu na kipa yupo chini, Makambo aliurukia kwa nia ya kuukwamisha wavuni, lakini mpira uliopigwa ukapaa juu ya lango la Mbeya City.

Mbeya City ilijibu shambulizi hilo dakika ya 18, wakati Paul Nonga alipoambaa na mpira na kuingia ndani ya eneo la hatari la Yanga, mpira ukamuendea Eliud Ambukile ambaye alipiga shuti lililotoka pembeni kidogo mwa lango, huku kipa Djigui Diarra akiwa amesimama.

Makambo aliwanyanyua wanachama, mashabiki na viongozi wa Yanga waliokuwa kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya alipopachika mpira ndani ya wavu kwa shuti lililogonga nguzo ya ndani, kabla ya mabeki wa Mbeya City kuusindikiza wenyewe dakika ya 39.

Ilikuwa ni kazi nzuri iliyofanywa na Khalid Aucho ambaye alipiga pasi ndefu iliyomkuta mfungaji, mabeki wa Mbeya City wakiwa wamepotea na kudhani mfungaji alikuwa ameotea.

Dakika chache kabla ya mapumziko, wenyeji walipata pigo baada ya beki wake Mpoke Mwakenyuke kuzawadiwa kadi nyekundu ya moja kwa moja kwa kumkanyaga kwa makusudi Djuma Shaaban.

Dakika nne baada ya mapumziko, Mbeya City ilipata mkwaju wa penalti, baada ya krosi iliyopigwa na Jamal Dulaz kutua kwenye mkono wa Mwamnyeto.

Alikuwa ni Joseph Ssemuju aliyeukwamisha wavuni na matokeo hayo yakasimama hadi dakika 90.

Kipindi cha pili, pamoja na kuwa pungufu, Mbeya City ilisimama imara kuzuia mashambulizi ya Yanga, pamoja na kushambulia kwa kushtukiza, kiasi cha kuonekana kama idadi ya wachezaji ni sawa.

Kwenye Uwanja wa Ushirika mjini Moshi, wenyeji Polisi Tanzania walidunguliwa bao 1-0 dhidi ya Geita Gold.

Raymond Massota ndiye aliyeuweka mpira ndani ya wavu dakika ya nane, baada ya kumegewa pande kutoka kwa George Mpole.

Coastal Union nayo ikiwa nyumbani, Uwanja wa Mkwakwani Tanga ilikubali kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar.

Ni kona iliyopigwa na David Luhende dakika ya 14, ikienda moja kwa moja wavuni na kumuacha kipa Mussa Mbisa na mabeki wake wakitupiana lawama.

# Simba SC kumwagilia moyo Mbeya

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Simba ambacho kimevuliwa ubingwa wa Tanzania Bara, leo kinajitupa kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya kucheza dhidi ya Prisons, ikiwa ni mechi ya raundi ya 29 ya Ligi Kuu.

Haitakuwa mechi muhimu sana kwa Simba, lakini kwa wenyeji Prisons itabidi icheze kufa au kupona kupata ushindi kwa ajili ya kujiondoa kwenye janga la kushuka daraja ambalo linaonekana kuwanyemelea.

Mechi hiyo inachezwa siku moja tu kwenye uwanja ambao Mabingwa Wapya wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga walicheza dhidi ya Mbeya City na kukabidhiwa kombe lao la ubingwa na mwanzo wa sherehe ukaanza kufanyikia hapo.

Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Selemani Matola amesema ni mechi ambayo anatoa nafasi kwa wachezaji wake kuonyesha uwezo wao, hasa kwa wale ambao muda mrefu walikuwa hawachezi.

Kwa mujibu wa Meneja Habari na Mawasiliano, Ahmed Ally amezitaja mechi zilizobaki kuwa ni za 'kumwagilia moyo', akiwa na maana ni za kuonyeshana upendo kati ya Wanasimba wenyewe kwa wenyewe, wanachama kwa mashabiki, mashabiki kwa wachezaji na wachezaji kwa wanachama na mashabiki, pamoja na viongozi kwa mashabiki.

Simba iko kwenye nafasi ya pili ikiwa na pointi 60, huku Prisons ikiwa nafasi ya 14 ikiwa na pointi 26.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >